




**Salim** shujaa Simba ikibeba Ngao Tanga

UKURASA 24




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Agosti 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581402


www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Slaa akamatwa

• **Wakili** wake ateta na Nipashe; Kamanda Muliro asema... *Endelea ukurasa wa 2*



Wakili Boniface Mwabukusi Dk. Wlibrod Slaa Mdude Nyagali

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**PM: WATAKAOIBA PEMBEJEO KUKIONA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza watendaji wote watakaobainika kuiba pembejeo za kilimo wachukuliwe hatua...

UKURASA WA 3

**MWINYI AIPONGEZA CRDB KUIMARISHA AFYA**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Benki ya CRDB kwa...

UKURASA WA 8

**KESI KUMWUNGUZA MTOTO YAANZA KUSIKILIZWA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeanza kusikiliza kesi inayomkabili mkazi wa Nyarugusu, Mathias Daudi (31)...


KUPISHA HIFADHI

## Fidia bilioni 26/- yaibua shangwe wakazi Mbarali

UKURASA 19



UKURASA 3

## Machinga washtukia jambo ugawaji maduka mapya ya biashara Mwenge

MICHEZO UTAWALA KIJESHI NIGER WATISHIA KUMUUA RAIS UK.19 KATUNI UK.6



Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari, Prof. Kenneth Bengesi (katikati), akishirikiana na Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan (wa pili kulia) pamoja Meneja Mkuu wa Kitengo cha Uendeshaji Afrika na Kimataifa wa Mahindra, Sandresh Parab (wa pili kushoto), kukata utepe kuzindua kituo cha mashine za kilimo (matrekta) jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sarga Motocorp, Sandeep Singh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Slaa akamatwa akiwa nyumbani kwake

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA Balozi wa Tanzania huko Sweden, Dk. Wilbroad Slaa, anadaiwa kukamatwa na Jeshi la Polisi nyumbani kwake Mbweni, Dar es Salaam jana kutokana na tuhuma ambazo hazijawekwa wazi.

Kiongozi huyo amekamatwa ikiwa ni siku moja tangu kukamatwa kwa Wakili Boniface Mwabukusi na Nyagali Mpaluka, maarufu Mdude, ambao walitiwa mbaroni walipofika Mikumi mkoani Morogoro, wakielekea Dar es Salaam.

Dickson Matata, Wakili wa Dk. Slaa, aliiambia Nipashe jana kwa simu kuwa mteja wake alikamatwa nyumbani na watu waliojitambulisha kuwa ni askari polisi.

Alisema wanaendelea kufuatilia kituo cha polisi alikopelekwa na kufahamu makosa yaliyosababisha kukamatwa.

"Ni kweli amekamatwa na watu waliojitambulisha kuwa ni polisi waliofika nyumbani kwake na hapa sasa hivi tunafuatilia kujua kituo alichopelekwa na makosa yake ni nini," Wakili Matata alifafanua.

Juzi Wakili Mwabukusi akiwa na Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kusini, Emmanuel Masonga na Mdude, walikamatwa na Jeshi la Polisi wakiwa Mikumi, mkoani Morogoro saa nane na nusu usiku kwa kile kilichoelezwa baadaye na jeshi hilo kuwa ni kutoa maneno ya uchochezi.

Kukamatwa huko kwa Dk. Slaa na wenzake kumekuja ikiwa ni siku chache tangu Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura kuonya kuhusu watu aliodai wanaandaa maandamano ya kuipindua Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, akiwataka kusitisha mpango huo kwa kuwa jeshi hilo halitowafumbia macho kwa kitendo hicho.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro alipopigiwa simu na Nipashe jana kuzungumzia taarifa za kukamatwa Balozi Dk. Slaa, alisema: "Kama kuna taarifa kama hiyo, tutawaambia, si huwa tunawaita? Basi tutawapatia."

Katika siku za karibuni, Dk. Slaa na Wakili Mwabukusi wamekuwa mstari wa mbele kukosoa serikali kuhusu mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai kupitia uwekezaji wa Bandari za Tanzania ambao ulikwishajadiliwa na kupitishwa na Bunge, wakidai mkataba huo hauna maslahi kwa wananchi.

Wiki iliyopita majaji watatu; Jaji Danstan Ndunguru ambaye alikuwa kiongozi wa jopo, Jaji Mustafa Ismail na Jaji Abdi Kagomba, waliosikiliza kesi kuhusu mkataba huo Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, walisema hoja tano kati ya sita zilizowasilishwa mahakamani kupinga Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii kati ya Tanzania na Dubai (IGA) wa Bandari, hazikuwa vinahusu ukiukwaji wa katiba.

Walisema mkataba huo unaolenga kuendesha, kuwekeza na kuendeleza bandari nchini, haukukiuka vifungu vya katiba, hivyo shauri halina mashiko. Linatupiliwa mbali.

Baada ya uamuzi huo, Wakili Mwabukusi alisema watafungua shauri katika Mahakama ya Rufani na wanapanga kuhamasisha maandamano yasiyo na kikomo.

Mkataba wa DP World na Tanzania ulitiwa saini Oktoba mwaka jana. Juni 5 mwaka huu, azimio la mkataba huo lilipitishwa na Bunge.

# Waziri Mkuu: Watakaobainika kuiba pembejeo washughulikiwe

**Na Mwandishi Wetu,** TANDAHIMBA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza watendaji wote watakaobainika kuiba pembejeo za kilimo wachukuliwe hatua za kisheria kwa kuwa wanaihujumu serikali.

Pia amemwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Tandahimba, Deogratius Mbowe, amhoji Ofisa Kilimo wa Kata ya Kitama, Sharaf Manjavila kwa tuhuma za kuchukua pembejeo za wakulima.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana alipozungumza na wananchi baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kitama, wilayani Tandahimba.

Baadhi ya wananchi walimwomba Waziri Mkuu 'aondoke' na Ofisa Kilimo huyo kutokana na kutoridhishwa na utendaji wake ikiwamo kumtuhumu kuiba pembejeo za wakulima wa korosho.

Wakulima hao walidai kuwa walifanyiwa uhakiki na kupewa namba, lakini wanapokwenda kuchukua pembejeo wanaambiwa hawajasajiliwa na majina yao hayajarudi, hivyo hawapewi dawa.

"Mashamba tulihakiki na namba tulipewa, tukifuata dawa tunaambiwa jina halijarudi na ukipeleka malalamiko yako makao makuu, unaambiwa ulishachukua dawa, tatizo letu ni bwana shamba hafai," alidai mmoja wa wananchi hao.

Waziri Mkuu aliwahakikishia wananchi hao kuwa serikali itahakikisha suala hilo linasimamiwa vizuri, hivyo waendelee kuiamini na kushirikiana nayo.

Majaliwa pia alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba kwa kushirikiana na Ofisa Kilimo Wilaya wasimamie ugawaji pembejeo katika wilaya hiyo.

Awali Waziri Mkuu alikagua uongezaji thamani korosho katika Kiwanda Organic Growth Limited (OGL) kilichoko wilayani Tandahimba.

Alisema kiwanda hicho kitakapokamilika, kitaongeza thamani ya zao hilo kwa kuwa wakulima watapata fursa ya kwenda kubangua korosho zao na kuuza ikiwa imeongezwa thamani.

Waziri Mkuu alimpongeza mwekezaji huyo mzawa kwa uamuzi wake huo kwa kuwa ujenzi wa kiwanda hicho unakwenda kuwapa wakulima soko la uhakika wa korosho zao.

Mkurugenzi wa Kiwanda hicho, Aldina Fakiri, alisema kitakuwa na uwezo wa kubangua tani 3,000 za korosho ikiwa ni sawa tani 720 za korosho zilizobanguliwa kwa mwaka.

Alisema kiwanda ambacho kipo katika hatua za majaribio, ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 3.5. Kinatarajiwa kutoa ajira 200. Kati yake, 50 ni za kudumu na 150 zitakuwa za muda.

# JK ahimiza amani kwa maendeleo ya SADC

**RUANDA,** ANGOLA

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, amezitaka nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kuhimiza amani ambayo ndio ngao ya maendeleo na kichocheo cha kuinua uchumi.

Kikwete aliyasema hayo juzi jijini Ruanda, Angola alipowasilisha mada kuhusu amani na usalama kama kigezo cha msingi cha kufikia maendeleo ya kweli kusini mwa Afrika.

Alisema amani na usalama ni maneno yenye dhana pana, tofauti na watu wengi wanavyoelewa ni kuwa huru na migogoro inayotumia silaha.

"Amani na usalama ni dhana pana inayojumuisha mambo mengi kama vile elimu, afya na ustawi wa jamii," alisema Kikwete.

Pia alitoa hadhari kwamba amani na usalama ni msingi wa maendeleo kwa SADC, na itakapokosekana mahali popote pale, watu wasitarajie kupata maendeleo.

Katika mkutano huo, alitolea mfano wa nchi zilizokuwa na migogoro ya kisiasa kwa muda mrefu kama Angola na Msumbiji namna zilivyoathirika kiuchumi hadi hapo ufumbuzi ulipopatikana.

Alisema utatuzi wa migogoro kwa njia ya amani na mazingira tulivu yaliyopo hivi sasa, imeshuhudiwa mataifa mengi ya kusini mwa Afrika yanapiga hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Taifa lisilokuwa na amani haliwezi kufanya mambo mengi ya kiuchumi na kuiletea nchi yake maendeleo kama vile biashara, kuvutia uwekezaji kutoka nje na hata ndani ya nchi, kujenga miundombinu kama barabara, shule na vituo vya afya kwa sababu fedha zote ambazo serikali inazipata, zinatumika kununua silaha kwa ajili ya kujilinda.

"Nchi za SADC zishirikiane kuhamasisha amani katika nchi zao, amani itaziwezesha serikali zao kujiamini na hatimaye kuwa na utawala bora, utawala wa sheria na kutoa haki kwa watu wote," alisema Kikwete, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jopo la Wazee wa SADC.

Viongozi wengine walioungana naye kuwasilisha mada katika mkutano huo ni Waziri Mkuu mstaafu wa Msumbiji, Luisa Diogo na Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani wa Angola, Balozi Joao Bernardo de Miranda ambao walwasilisha mada kuhusu miundombinu inayohitajika kuunganisha SADC na hali ya sasa ya dunia na athari zake kwa jumuiya hiyo.


IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI

LAND CASE NO.13 OF 2022

DAUDI BASHE HASSAN ..................PLAINTIFF
(As the Administrator of Estate of the late Asha Mohamed Laban)

VERSUS

MICROFOOD LIMITED ..................1st DEFENDANT
T.I.B DEVELOPMENT BANK LTD..................2nd DEFENDANT
THE ATTORNEY GENERAL..................3rd DEFENDANT

TO MICROFOOD LIMITED
P.O.BOX 1483-MOSHI

NOTICE FOR MENTION,

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 13th day of September,2023 at 9:00 a.m. before Honourable Judge A.P. KILIMI.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this **7th day of August 11, 2023,**

Deputy Registrar
Moshi



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA KATA
FOMU YA KUITWA SHAURINI
KYELA WILAYA YA KYELA
SHAURI LA MADAI NAMBA 70 LA MWAKA 2023

JUDITH JASTON EVARIST
DHIDI YA
AXACID A. MBWILE

POPOTE ULIPO
Unajulishwa kwamba shauri lililotajwa hapo juu litasikilizwa siku ya IJUMAA Tarehe 18 Mwezi 08 Mwaka 2023 Saa 3:30 Asubuhi katika ofisi ya MOSEM karibu na Shule ya Msingi KUELA hivyo unatakiwa kuwepo kwa ajili ya OMBI LA KUACHANA (TALAKA) baada ya kutelekezwa bila huduma na Watoto Wnne zaidi ya miaka kumi (10) Wakati wa kusikiliza shauri hilo katika tarehe iliyotajwa.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Baraza la kata hii leo Tarehe 07 mwezi 08 Mwaka 2023



Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, akiwasilisha mada kuhusu amani na usalama katika nchi za Kusini mwa Afrika juzi, nchini Angola kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Wengine ni Waziri Mkuu mstaafu wa Msumbiji, Luisa Diogo (kulia) na Katibu Mtendaji wa zamani wa SADC, Tomaz Salomão. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machinga washtukia jambo ugawaji maduka mapya ya biashara Mwenge

**Na Waandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wadogo, maarufu machinga, waliokuwa wanafanya biashara eneo linalojengwa stendi mpya ya Mwenge, wilayani Kinondoni, wameikumbusha serikali kutimiza ahadi iliyoitoa ya kuwapa kipaumbele wakati wa kugawa maduka kwa ajili ya biashara baada ya ujenzi kukamilika.

Pia wamedai wanaona dalili serikali kuwatenga na kuwapa vibanda hivyo wafanyabiashara wakubwa, jambo wanalodai ni kinyume cha makubaliano ya awali wakati ujenzi unaanza mwaka 2018.

Katika mazungumzo na Nipashe wiki iliyopita, wafanyabiashara hao waliomba serikali kutowadharau kutokana na biashara wanazofanya kwa kuwa uwezo wa kulipia vibanda hivyo wanao kama wakipewa nafasi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyabiashara hao, Salvatory Apolnary, alikumbusha kuwa mwaka wa fedha 2018/19, serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni iliwaomba kupisha ujenzi wa mradi wa kituo cha magari katika eneo hilo na kuwahidi kupewa kipaumbele kupata majengo ya biashara mradi ukikamilika.

Nipashe iliona nakala ya barua kutoka Halmashauri ya Kinondoni ambayo baadhi ya maneno yake yanaeleza "unatakiwa kupisha mradi wa ujenzi na baada ya kukamilika utatakiwa kufika na barua hii Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ili uweze kukabidhiwa eneo lako la biashara."

Apolnaty alisema kuwa ahadi hiyo pia ilisisitizwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Aprili mwaka jana alipokwenda kukagua maendeleo ya mradi huo, hivyo kuwapa matumaini kuwa watapata eneo lenye hadhi la kufanyia biashara zao.

Alisema kuwa baada ya kubaini ukimya, Juni mwaka huu waliandikia barua kwenda halmashauri kukumbusha uzingatiaji wa kupewa maduka kama walivyoahidiwa, lakini walijibiwa kuwa hawatambuliki na kutakiwa kujisajili katika mfumo wa TAUSI na kufuata utaratibu wa kuomba vibanda kama watu wengine.

Alisema pia walishangazwa na kauli ya Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila alipokwenda kukagua mradi huo akiongozana na uongozi wa halmashauri mwezi uliopita, kuwa barua walizopewa zenye taarifa ya kupewa kipaumbele ni za kisiasa, hivyo wanatakiwa kufuata utaratibu wa kuomba nafasi pamoja na wafanyabiashara wengine.

"Kwa kweli kauli ile ilitukatisha tamaa, kwamba inakuwaje wengine wanatoa ahadi ya wao kupewa kipaumbele lakini mwingine anakuja kusema ni maneno ya kisiasa. Piga picha vibanda vipo takribani 144 tu tukiomba wafanyabiashara wote hapa Dar es Salaam sisi tutapata nafasi kweli?

"Ni kama vile wametudharau kutokana na biashara zetu tunazofanya, wanaona hatuna uwezo wa kulipia kodi katika vibanda hivyo, wanataka kuwapa," alisema. Mmoja wa wafanyabiashara hao anayeuza viatu vya kike, Mabinduzi Wilson, alisema kitendo cha serikali kuwaambia wakajiandikishe katika mfumo wa kielekroniki wa TAUSI bila kuwapa elimu yoyote ya kutumia mfumo huo, kinalenga kuwanyima vibanda hivyo na kuwapa watu wengine.

Mfanyabiashara wa nguo za kike, Farida Helman, alisema serikali itakuwa haijawatendea haki kuwanyima vibanda hivyo kwa kuwa walishirikiana vyema na serikali ikiwamo kulinda miundombinu wakati wote wa ujenzi.

Frida ambaye awali alikuwa na kibanda alichokodishwa na Chama cha Mapinduzi (CCM), alisema amefanya biashara tangu miaka ya 1980 katika eneo hilo na kuitaka serikali iwaangalie kwa jicho la kipekee.

Akizungumzia madai hayo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Manispaa ya Kinondoni, Aquilinus Shinduki, alisema manispaa imebadilisha utaratibu wa upangishaji wa vibanda vyake na sasa unafanyika kwa njia ya mnada.

Alisema mpango huo ni maelekezo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa hamashauri zote nchini na uliridhiwa na vikao vya madiwani na kutangazwa kupitia vyombo vya habari Mei mwaka huu.

Alisema lengo la utaratibu huo mpya ni kuwapa nafasi sawa wafanyabiashara wote nchini wenye nia ya kukodisha vibanda hivyo na kuondoa malalamiko ya upendeleo na mazingira ya rushwa.

"Kwahiyo, hapo wafanyabiashara wenyewe watashindana, na mfumo ndiyo utaochagua mwenye dau kubwa. Kwahiyo, tunaendelea kuwasisitiza wafanyabishara wote nchini wanaotaka kukodisha vibanda hivyo kujisajili katika mfumo wa TAUSI," alisema. Kuhusu elimu ya namna ya kujisajili kwenye mfumo huo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Hanifa Hamza, alisema walimekuwa wakiitoa kwa wafanyabiashara hao mara kwa mara.

"Elimu imetolewa vya kutosha na wengi wanapiga simu wanaelekezwa namna ya kutumia mfumo," alisema.

**Imeandaliwa na Jenifer Gilla, Emmaloveness Gaston na Mwanahamisi Mussa (TUDARCo)**

# Rais Dk. Mwinyi aipongeza CRDB kuimarisha afya

**Na Maria Semi**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Benki ya CRDB kwa mikakati yake katika kuboresha afya nchini, akizitaka kampuni zingine binafsi kujitoa ili kuongeza nguvu kwa kuwa mahitaji ni makubwa.

Alitoa pongezi hizo jana katika kilele cha CRDB Bank Marathon kilichofanyika Agosti 13 katika viwanja vya The Green vilivyoko Oysterbay jijini Dar es Salaam na kuwashuhudia washindi wakiondoka na zawadi nono baada ya kuonyesha kasi kubwa kuliko wakimbiza upepo wengine zaidi ya 7,000 waliojitokeza na kushiriki.

Akieleza mchango wa CRDB Bank Marathon katika sekta ya afya, Rais Dk. Mwinyi alisema ni mkubwa na unagusa pande zote za Muungano kwa kuwawezesha wasio na uwezo wa kugharimia matibabu yao pamoja na kuimarisha miundombinu.

"Fedha zinazokusanywa kutoka kwa washiriki wa mbio hizi za hisani, zinaelekezwa kwenye matibabu ya watoto wenye matatizo ya moyo pamoja na wanawake wenye ujauzito hatarishi.

"Mwaka huu fedha hizi zitajenga kituo cha afya kule Zanzibar. Huu ni mchango mkubwa unaowagusa Watanzania wengi. Ninawaomba wadau wengine nao waone namna wanavyoweza kushirikiana na serikali kuboresha huduma za afya," Rais Dk. Mwinyi alisema.

Hata kuratibu mbio hizi zilizokusanya Sh. bilioni moja zitakazoelekezwa kwa walengwa waliokusudiwa mwaka huu, Rais Dk. Mwinyi alisema kulihitaji ushiriki wa watu wenye nia moja na akaipongeza kampuni ya Sanlam Insurance ambayo ndio mdhamini mkuu wa mwaka huu.

"Benki ya CRDB inashirikiana na washirika wake kufanikisha mbio hizi. Niwapongeze kampuni ya Sanlam ambao niliwaona Ikulu kule Migombani, Zanzibar. Hongereni Sanlam kwa kuwa sehemu ya mchango huu mkubwa kwa jamii," alipongeza.

Akieleza namna mbio za CRDB Bank Marathon zinavyoigusa jamii, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kwa misimu mitatu iliyotangulia, fedha zilizokusanywa kutokana na usajili wa washiriki na zile zilizochangwa na washirika, zimewagusa watu wengi.

"Mwaka 2020 wakati tunaanza, zaidi ya watu 4,000 walishiriki na kufanikisha kukusanya Sh. milioni 200 zilizofanikisha upasuaji wa moyo kwa watoto 100 katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) pamoja na programu ya utunzaji mazingira ya Pendezesha Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa mwaka 2021 kulikuwa na washiriki 5,000 na jumla ya Sh. milioni 350 zilikusanywa ambazo zilitumika katika upasuaji wa moyo kwa watoto wengine 100 na kujenga Kituo cha Mawasiliano katika Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI).

Alifafanua kuwa mwaka jana, jumla ya Sh. milioni 470 zilikusanywa kutoka kwa washiriki 6,000 ambazo zilitumika katika gharama za matibabu ya wagonjwa watoto 100 JKCI na wanawake wenye ujauzito hatarishi na walio na maradhi ya fistula katika Hospitali ya CCBRT.

Kutokana na mafanikio hayo, Nsekela alisema msimu huu wa nne wa CRDB Bank Marathon una malengo makuu manne ambayo ni kujenga kituo cha afya ya mama na mtoto visiwani Zanzibar, kuchangia matibabu ya watoto wenye matatizo ya moyo, kuchangia matibabu ya wanawake wenye ujauzito hatarishi na wanaougua fistula pamoja na kuendelea programu ya Pendezesha Tanzania kwa kuimarisha bustani za Zanzibar ikiwamo Bustani ya Jamhuri, Bustani ya Migombani-Botanic Garden, Bustani ya Tenga-Mnazi Mmoja, Bustani ya Mbele ya Ikulu Migombani pamoja na Njia Nne za Michenzani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa CRDB Bank Foundation, Martin Warioba, alisema mafanikio ya mbio wanazoziratibu waliyoyapata ndani ya miaka mitatu iliyopita, yamevuka mipaka kwa kuwa katika mwaka wa pili tu mbio hizo zilitambulika kimataifa na Chama cha Usajili na Upimaji wa Mbio za Kimataifa (AIMS) na Shirikisho la Kimataifa la Michezo wa Riadha (World Athletics).

"Hii si tu imekuwa ni heshima kwa benki yetu, bali pia ni heshima kwa nchi yetu.

TOL Gases Limited
We Deliver
Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

# BOARD MEMBER VACANCY.

TOL Gases Limited is the leading manufacturer and distributor of Industrial and Medical Gases. Additionally the Company distributes high quality brands of welding and related consumables as well as medical oxygen related appliances within Tanzania and the neighbouring countries through distributorship arrangements.

The secretariat of the Board of Directors of TOL Gases Limited, do hereby invite shareholders to nominate suitable candidates to be elected to fill **one vacant position of Board Membership. Female Nominees are strongly encouraged.**

**Requirements:**

1. Expertise/Skills in Governance, Risk, Compliance and Administration.

2. Applicants are required to be nominated / proposed by a Shareholder who is duly qualified to be present and vote at the meeting and has signed the proposition to concede his/her willingness to be elected.

3. Any shareholder who would like to nominate / propose a person for election to fill the Board Membership position, may submit the following to the Secretary not later than 20th August 2023 :-
   - Notice of his/her intention to propose such a person signed by the proposed person conceding his willingness to be elected.
   - Resume of the proposed person with due consideration to the requirements of the Companies Act and the Company's MEMARTS.

4. Submission should be delivered to the following address.

**Company Secretary**
**TOL Gases Limited**
**Plot 4b, Nyerere Road**
**P. O. Box 911,**
**Dar es Salaam**
**Email: nlulu@tol-gases.co.tz**
**mjuliana@tol-gases.co.tz**

217549901

Directors: S. Mponji – (Tanzanian) – Chairman, J. Massawe – (Tanzanian), S. Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian), L.C. Kitoka – (Tanzanian).

TOL Gases Limited
We Deliver
Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

# NOTICE

## 28TH ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** the 28th Meeting of the Shareholders of TOL Gases Limited will be held on a hybrid of physical attendance at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) and via ZOOM video conferencing on 25th August, 2023 at 9.00a.m to transact the following business:-

1. Adoption of the Agenda.
2. Confirmation of Minutes of the year 2021 Annual General Meeting held on 19th August, 2022.
3. Matters arising from minutes of the year 2021 Annual General Meeting.
4. Chairman's Statement.
5. To receive Directors' Report, Auditors' Report and the Audited Financial Statements for the year ended December, 31, 2022.
6. To approve Dividend Payment.
7. To approve Directors' Fees.
8. To appoint Auditors for the year 2023.
9. Election of Directors.
10. To set the place, date and venue of the next meeting.
11. Any other business (Duly notified at least seven days before the meeting)

Registration for participating in the ZOOM Video Conferencing should be done through phone no **0685750201/0685750203.**

member entitled to attend and vote at the Meeting is also entitled to appoint a proxy (whether a member of the Company or not) to attend and vote in his/her stead.

All proxy forms or letters appointing proxy must be lodged at the office of the Company Secretary at least 48 hours before the time fixed for the holding of the meeting or via email to **mjuliana@tol-gases.co.tz/nlulu@tol-gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**
**COMPANY SECRETARY**

217549901

Directors: S. Mponji – (Tanzanian) – Chairman, J. Massawe – (Tanzanian), S. Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian), L.C. Kitoka – (Tanzanian).

TANGAZO

TOL Gases Limited
We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## EXTRACT OF THE STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2022

| | 2022<br>TZS '000 | 2021<br>TZS '000 |
|---|---|---|
| Revenue | 25,558,350 | 24,849,905 |
| Cost of sales | (13,746,778) | (14,532,314) |
| **Gross profit** | **11,811,572** | **10,317,591** |
| Other income | 161,109 | 28,999 |
| Operating expenses | (4,631,715) | (4,877,395) |
| Trade receivables impairment release | (9,544) | - |
| **Operating profit** | **7,331,422** | **5,469,195** |
| Finance costs | (1,134,852) | (991,084) |
| **Profit before tax** | **6,196,570** | **4,478,111** |
| Income tax expense | (2,716,334) | (1,183,480) |
| **Profit for the year** | **3,480,236** | **3,294,631** |
| Other comprehensive income | - | - |
| **Total comprehensive income** | **3,480,236** | **3,294,631** |
| Earnings per shares (TZS) | | |
| – Basic | 60.52 | 57.29 |
| – Diluted | 60.52 | 57.29 |

## EXTRACT OF STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2022

| | 2022<br>TZS '000 | 2021<br>TZS '000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Non-current Assets** | | |
| Property, plant and equipment | 36,086,300 | 26,927,827 |
| Right-of-use assets | 328,068 | 335,125 |
| Intangible asset | 225,258 | 296,478 |
| Advances to suppliers | - | 446,856 |
| | **36,639,626** | **28,006,286** |
| Current assets | | |
| Inventories | 2,337,579 | 4,089,520 |
| Trade and other receivables | 6,879,076 | 5,019,850 |
| Cash and bank balances | 5,098,300 | 4,312,902 |
| Asset held for sale | 2,674,275 | 2,674,275 |
| Advances to suppliers | 2,370,249 | 923,077 |
| | **19,359,479** | **17,019,624** |
| **TOTAL ASSETS** | **55,999,105** | **45,025,910** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| **Equity** | | |
| Share capital | 5,750,596 | 5,750,596 |
| Share premium | 6,762,049 | 6,762,049 |
| Retained Earnings | 12,937,553 | 11,757,384 |
| | **25,450,198** | **24,270,029** |
| **Non-current liabilities** | | |
| Long term borrowings | 8,813,437 | 11,927,120 |
| Lease liabilities | 59,627 | 59,817 |
| Deferred tax liability | 3,878,562 | 3,387,620 |
| | 12,751,626 | 15,374,557 |
| **Current liabilities** | | |
| Trade and other payables | 3,721,310 | 2,115,619 |
| Lease liabilities | 11,386 | 11,385 |
| Tax payable | 1,004,532 | 208,976 |
| Bank overdraft | 7,350,103 | - |
| Cylinder deposits | 517,137 | 497,464 |
| Current portion of loans | 5,192,813 | 2,547,880 |
| | **17,797,281** | **5,381,324** |
| Total liabilities | **30,548,907** | **20,755,881** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **55,999,105** | **45,025,910** |

217549902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Pazia Bara linapofunguliwa kesho, 'Fair Play' muhimu*

**PAZIA** la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa mwaka 2023/2024, linatarajia kufunguliwa rasmi kesho kwa timu sita kushuka kwenye viwanja mbalimbali nchini ili kusaka ubingwa wa ligi hiyo unaoshikiliwa na Yanga ya Dar es Salaam.

Mechi za ufunguzi zitakuwa ni Ihefu dhidi ya Geita Gold, Namungo watawakaribisha JKT Tanzania na Coastal Union ya Tanga wataifuata Dodoma Jiji FC.

Msimu mpya unaanza huku kila timu ikijinasibu imesajili kikosi kizuri na ziko tayari kwa safari ya miezi nane kusaka mfalme mpya wa soka lakini kusaka nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kwa mashabiki wa soka hapa nchini kipindi cha kufuatilia burudani kimefika, lakini kipindi cha utani na maneno ya kukera kwa upande wa wapinzani kitaanza kukoleza kasi yake.

Lakini kuelekea kwenye msimu mpya utakaoanza kesho, lazima tugusie mambo kadhaa ambayo mashabiki wa soka na wapenzi wa kila timu inayoshiriki Ligi Kuu Bara wanatarajia kuona.

Klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu zilipata nafasi ya kufanya usajili na kuimarisha vikosi vyao kuelekea msimu mpya na tunaamini makocha walifanya usajili kulingana na mahitaji yao.

Lakini mbali na kupata muda wa usajili, pia kila timu ilipata muda wa kujiandaa, zipo zilizoenda kuweka kambi ya 'Pre-season' nje ya nchi, zipo zilizohama mikoa yao na kwenda mikoa mingine, lakini zipo zilizoweka kambi ndani ya mikoa yao, yote hii ni kutafuta maandalizi bora na kuvijenga vikosi.

Tunaamini sasa mashabiki na wadau wa soka wataona ligi bora, ligi yenye ushindani na kuleta msisimko mkubwa.

Tayari ligi yetu imeanza kupata umaaarufu mkubwa na kupanda katika viwango vya ubora, hivi karibuni ligi yetu imetajwa kuwa ligi ya tano kwa ubora Afrika, sasa vilabu vyetu vionyeshe kweli ubora huo kwa kuongeza ushindani katika mbio za ubingwa msimu huu.

Tunazisihi timu zetu, wachezaji, makocha na viongozi kuziandaa timu zao kuonyesha ushindani wa kweli, si tu kusaka ubingwa na timu zinazosaka tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa kuwa na sifa stahili, lakini kuendelea kuipa ubora ligi yetu ili itoke kwenye nafasi ya tano iliyotangazwa na kupaa hadi 'top three' ya Afrika.

Hata hivyo kuifanya ligi yetu kuwa bora na yenye ushindani si jukumu la klabu peke yake, pia mashabiki wana nafasi yake na Shirikisho la Soka Nchini (TFF).


Kwa mashabiki wanatakiwa kuendelea kujitokeza kwa wingi viwanjani kushangilia timu zao na kuwapa hamasa wachezaji wao waweze kufanya vizuri, lakini TFF, kusimamia kanuni na haki kupitia kamati zake mbalimbali zinazosimamia ligi hiyo pamoja na ligi nyingine zilizoko chini yake.

Hatutarajii kuona makosa ya mchezaji au kiongozi yanafanyika wiki hii na uamuzi wake kutolewa baada ya miezi mitatu kwa waliofanya makosa kuendelea kuhudumia timu zao.

Kwa muda sasa suala la uamuzi taratibu baadhi ya makosa ya wazi yaliyokuwa yanafanywa na waamuzi yameanza kupungua, hata hivyo ni lazima tuweke mkazo, waamuzi wahakikishe wanatenda haki na kupunguza makosa yanayoitwa ya kibinadamu kwa upande wa timu 'ndogo' huku wakiwafaidisha 'vigogo'.

Mwisho, tunazitakia klabu zote za ligi kila la heri kwenye safari ya kusaka bingwa mpya wa msimu wa 2023/2024, lakini tunazitakia msimu bora zaidi ya uliopita.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Mashabiki, klabu zijiandae na ligi, si kulalamikia ratiba*

Na Adam Fungamwango

**BAADA** ya ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara kutolewa, baadhi ya mashabiki wanaojiita kindakindaki au 'wafia timu' wa klabu mbalimbali wamejitokeza kuanza kulalamikia.

Mashabiki hao kila mmoja kwa upande wake wanadai ratiba haiibebi timu yake, badala yake inaikandamiza na kuwapendelea wenzake.

Sitowataja majina, lakini mmoja wa Simba alilalamika Yanga kuanzia mechi tatu mfululizo nyumbani, akadai ratiba hiyo inaibeba Yanga kwa sababu itaanza kukusanya pointi za mapema kabla ya kwenda ugenini.

Yanga itaanza dhidi ya KMC nyumbani halafu itakutana na JKT Tanzania na mchezo wake wa tatu itawakaribisha Namungo, michezo yote ikipigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mwingine wa Yanga akalalamika watani zao Simba wanaanza kwa kukutana na timu 'mchekea' ili wakusanye pointi za mapema, wao wakiwa wamepangiwa wapinzani wagumu.

Akaenda mbali zaidi na kudai wenzao Simba watamaliza mechi tatu za mwisho nyumbani, hivyo kama wakikusanya pointi kadhaa itakuwa rahisi kumaliza vizuri na kupata ubingwa ikiwa wanahitaji pointi chache. Simba itamaliza mechi tatu za mwisho nyumbani dhidi ya Geita Gold, KMC na JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Haya ndiyo malalamiko ya mashabiki wa soka wa timu hizi, lakini inawezekana kabisa wakawa wametumwa na klabu kuwasemea kwa sababu viongozi wanaogopa kujitokeza hadharani kulalamikia jambo kama hilo.

Dunia nzima huwa hakuna ratiba rafiki au adui kwa timu, badala yake zinapangwa kutokana na kamati kwa mpangilio maalum utakaoziwezesha timu zote kucheza mechi sawa za nyumbani na ugenini.

Timu zote zitacheza na timu zile zinazoitwa ngumu na mchekelea, hivyo sioni sababu ya kupigizana kelele.

Yule anayeona timu yake inaanza na timu ngumu hajiulizi kuwa baada ya kuzimaliza hizo ngumu ataanza kupata mechi nyepesi na wenzake sasa wataanza kucheza anazoziita ngumu.

Halafu ukiangalia ratiba hiyo, kama Yanga inaanza mechi tatu nyumbani, halafu Simba nayo mwisho wa msimu inamaliza tatu nyumbani kuna ubaya gani?

Hizi ni dalili tu za kujihami na woga, kwa sababu kama timu ina kikosi kizuri sidhani kama itashindwa kushinda mechi zake za ugenini.

Tumeona msimu kwenye ligi timu nyingi zikipata ushindi ugenini, tena hata zile zilizokuwa zikiitwa vibonde nazo zilishinda sana mechi zao za ugenini.

Malalamiko haya yakamsukuma Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, kueleza akizitaka timu kujiandaa kisawasawa kwa ajili ya Ligi Kuu msimu ujao kwani utakuwa mgumu.

"Nimesikia kuna watu wanalalamikia ratiba wamepangiwa mechi ngumu, wenzao rahisi, niwaambie tu kuelekea msimu ujao wa Ligi unaoanza Agosti 15, mwaka huu, timu zinazotakiwa kujiandaa kisawasawa kwa sababu hakutakuwa na mechi rahisi, timu zote zimesajili wachezaji wazuri, hivyo maandalizi mazuri ndiyo wanaweza kuipa timu ushindi," alisema Boimanda.

Akaongeza hakuna timu ambayo itacheza mechi zote nyumbani au ugenini, hivyo kujiandaa kucheza popote pale.

"Wengine wanasema wao wanaanzia nyumbani halafu baadaye watakuja kucheza ugenini, niseme tu ratiba imeshapangwa, timu zote haziwezi kucheza nyumbani, wala zote kwenda kucheza ugenini, baadhi zitabaki na zingine zitaondoka, kinachotakiwa ni kujipanga ili kucheza mechi zote, hakuna mchekea, ligi yenye ubora namba tano Afrika huwezi kupata timu dhaifu tena," akapigilia msumari.

Na mimi nashindilia hapo hapo kuwa watu wasianze kutafuta mchawi mapema ili timu zao zisipofanya vizuri wapate sababu.

Ligi haijaanza, kinachotakiwa ni kujipanga kukabiliana nayo, kila mechi kucheza kwa uzito sawa, iwe nyumbani au ugenini.

## Katibu Mkuu asifu utekelezaji mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi

**Na Robert Hokororo**, KISHAPU

NAIBU Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Switbert Mkama, ameridhishwa na usimamizi na utekelezaji wa Mradi ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo Ikolojia Vijijini (EBARR) katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga.

Alibainisha hayo alipozuru na kukagua mradi wa mashine za kukoboa na kusaga nafaka, madume ya ng'ombe aina ya borani na uchimbaji wa malambo katika vijiji vya Kilolelі na Muguda, wilayani Kishapu juzi.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa ziara hiyo, Dk. Mkama alitoa wito kwa wananchi wilayani humo kuitunza miradi hiyo ambayo inatekelezwa kwa lengo la kusaidia utunzaji wa mazingira na kukabiliana na ukame kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Ndugu zangu, ninaomba niwaambie miradi hii inayoletwa hapa kwenu na maeneo mbalimbali, itawasaidia katika kujipatia kipato kwa kufanya shughuli mbalimbali zikiwamo ufugaji nyuki zitakazowasaidia kuacha shughuli zinazoharibu mazingira ukiwamo ukataji miti na kuchoma mkaa na mkipata fedha mtanunua majiko banifu na ya gesi," alisema.

Dk. Mkama aliwahimiza viongozi na wananchi wilayani Kishapu kuhakikisha shughuli zote za mradi zinakamilika Desemba mwaka huu wakati mradi huo utakapofikia ukingoni pamoja na kuufanya kuwa endelevu ili kunufaisha vizazi vijavyo.

Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, aliishukuru serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutekeleza mradi wa EBARR. Umekuwa msaada mkubwa kwa wananchi wilayani Kishapu.

Alisema miradi mbalimbali ikiwamo malambo, mifugo, kiwanda kidogo cha uchakataji wa ngozi ambacho kinahusisha kikundi cha ushonaji wa viatu na unenepeshaji wa mifugo, unakwenda kuinua ufugaji wilayani hapa.

Mbunge huyo pia alisema mashine za kukamua alizeti zinazotarajiwa kutolewa kupitia mradi huo, zitawasaidia wakulima wa zao hilo kupata fursa ya kukamua mafuta na hivyo kuinua uchumi wa wilaya.

Shughuli hizo zinazotekelezwa kupitia mradi wa EBARR wilayani Kishapu, zinagharimu Sh. bilioni 1.6 ambapo unatekelezwa katika Kata ya Kilolelі inayohusisha vijiji vya Kilolelі na Muguda na Kata ya Lagana katika vijiji vya Mihama na Beledi.

Mradi huo unaofadhiliwa na Mfuko wa Nchi zinazoendelea kupitia Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF), unatekelezwa pia katika wilaya za Simanjiro (Manyara), Mvomero (Morogoro) na Kaskazini 'A' Unguja (Zanzibar).



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiangalia korosho zilizobanguliwa kwa ajili ya kuuzwa alipokagua na kuona juhudi za uongezaji thamani wa zao la korosho katika Kiwanda cha Organic Growth Limited wilayani Tandahimba mkoani Mtwara jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Aldina Azizi. **PICHA: OWM**

### UHABA WA AJIRA

# Mbowe akosoa mfumo wa elimu nchini

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MWENYEKITI wa Chama Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe ameitaka serikali kufanya maboresho ya mifumo ya elimu nchini ili vijana wanufaike na elimu hiyo kwa kupata fursa.

Mbowe alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki katika Maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani yaliyokwenda sambamba na kufungwa kwa kampeni ya +255 Katiba Mpya awamu ya pili iliyokuwa inafanyika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Licha ya kutambua mikakati mbalimbali inayofanywa na serikali kubadili mfumo wa elimu nchini, Mbowe alidai mfumo wa elimu nchini umekuwa wa kipaguzi na usiowaandaa vijana kama sehemu ya uzalishaji na elimu hiyo, hivyo kubaki kudharauliwa na majirani.

Alisema elimu inayotakiwa ni ile itakayozingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kuwafanya vijana kushindanishwa katika soko la ajira kimataifa wala. Alisema mitaala ya zamani haina faida katika mustakabali wa ajira.

"Lugha za kimataifa zitumike kuwatayarisha vijana katika soko la kimataifa ikiwa ni pamoja na kutumia nyenzo mbalimbali za taifa ikiwamo Kiswahili ili kuhakikisha vijana wanapata fursa ndani na nje ya nchi ili waache kutegemea vyanzo vya ajira vilivyozoeleka.

"Kama Taifa hatuwezi kujifungia kwa kutaka kutumia lugha ya Kiswahili katika ngazi zote za elimu, bali lazima tutoke kimataifa na kuhakikisha tunatumia fursa ya Kiswahili kuwainua vijana na kuwapa mwanga wa ajira kimataifa.

"Na hii siyo soko tu la ajira bali hata katika mashindano ya fursa za kimawasiliano kwa kutumia lugha mbalimbali za kimataifa na tunawaomba watanzania wote wanaoona umuhimu wa kuwapeleka vijana wao kusoma katika shule za Kiingereza wafanye hivyo.

"Kama serikali itashindwa kufanya hivyo, sisi CHADEMA tukiingia madarakani tutahakikisha tunabadilisha mitaala yote ya elimu na kukifanya Kiingereza kufundishwa katika mifumo yote ya elimu ikiwa ni pamoja na elimu ya awali ili kuwapa fursa vijana kuajirika," alisisitiza.

Awali baadhi ya vijana wa chama hicho waliomba uongozi wa chama hicho kuhakikisha wanaendelea kuwapigania vijana dhidi ya tatizo la uhaba wa ajira na fursa muhimu za kujiajiri.

Mwakilishi wa Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA) Kanda ya Nyansa ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza hilo Mkoa wa Iringa, Necto Kitiga, alisema ongezeko la vijana wanaomaliza vyuo vikuu, vyuo vya kati na masomo ya sekondari limeendelea kuwa kubwa zaidi nchini.

Aliitaja ni hali inayoongeza idadi ya vijana wasio na ajira ajira ndani ya serikali na sekta binafsi.

Mazingira ya kujiajiri yamekuwa siyo rafiki kutokana na miongozo waliyoiita siyo rafiki inayowekwa na serikali.

Alisema fedha zilizotakiwa kutumika kama sehemu ya mitaji ya vijana kutokana na asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri imekuwa haiwafikia vijana lengwa, hivyo kuomba kuwe na mkakati madhubiti kuhakikisha sheria mbalimbali na kanuni za mikopo hiyo zinafanyiwa marekebisho ili kuwanufaisha vijana wote.

"Na sisi vijana wakati tukiadhimisha siku yetu ulimwenguni, tunatuma ujumbe wetu kwa vijana wenzetu kuhakikisha wanashiriki katika kuomba katiba mpya inakayoleta mabadiliko katika mifumo ya kiutawala na kutoa fursa kwa vijana wa taifa hili," alisema Kitiga.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**





Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Iringa, Salim Asas, akiongea na wanachama kwenye kikao maalumu kilichowakutanisha wajumbe 700 wa Halmashauri Kuu zote za CCM za wilaya na mkoa kuhusu hali ya siasa katika mkoa huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi anayeshtakiwa kumwunguza mwanawe yaanza kusikilizwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeanza kusikiliza kesi inayomkabili mkazi wa Nyarugusu, Mathias Daudi (31) anayeshtakiwa kwa kumchoma mikono na maji ya moto mtoto wake - msichana mwenye umri wa miaka tisa na kumsababishia maumivu makali mwilini.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mwishoni mwa wiki mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Johari Kijuwile na aliposomewa shtaka lake, alikana kuhusika na kosa hilo na yuko nje kwa dhamana.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Venance Mkonongo, ulidai mahakamani huko kuwa kesi hiyo ilikuja kwa ajili ya kusikilizwa na una mashahidi wawili na uko tayari kuwasikiliza.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Kijuwile alikubaliana na ombi hilo na kumwuliza mshtakiwa kama yuko tayari kuwasikiliza mashahidi wawili wa Upande wa Jamhuri. Alidai yuko tayari.

Shahidi wa kwanza wa Upande wa Jamhuri, Andrea Lazaro (49) - Ofisa Usitawi wa Jamii Kata ya Nyarugusu, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkonongo, alidai kuwa Aprili Mosi 2023, alipata taarifa kutoka kwa Mwenyekiji wa Kijiji, Musa Siyote na kumwambia kuwa mtoto msichana mwenye umri wa miaka tisa amechomwa mikono na baba yake mzazi aitwaye Mathias Daudi.

Lazaro alidai mahakamani kuwa baada ya kupata taarifa hizo, alikwenda nyumbani kwa Daudi na alipofika, alimkuta Daudi na kumwuliza 'ni kweli wewe umemchoma mikono mtoto wako?' Daudi alijibu 'ni kweli nilimchoma mtoto wangu mikono kwa kumwagia maji ya moto'.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya Daudi kukiri kumchoma moto mwanawe huyo, alimwuliza 'huyo mtoto yuko wapi?' Alidai Daudi alimwambia kuwa baada ya kumchoma moto mwanawe, alichukuliwa na mama mdogo wake aitwaye Debora Abdallah.

Shahidi huyo alidai alimwambia Daudi ampeleke huko kwa



Mshtakiwa Mathias Daudi, akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita baada ya kesi inayomkabili kuahirishwa. **PICHA: JOCTAM NGELLY**

Debora ili akamwone huyo mtoto na kwamba mshtakiwa huyo alikubali kumpeleka hadi nyumbani kwa Debora.

Alidai kuwa walipofika nyumbani kwa Debora, alimkuta mtoto amechomwa kwenye viganja vya mikono yote miwili na hali yake ilikuwa mbaya.

Alidai kuwa kutokana na hali hiyo, aliwaambia wazazi wampeleke mtoto huyo hospitalini na badaye aliondoka na kurudi nyumbani kwake.

Aliendelea kudai mahakamani kuwa Aprili 3 mwaka huu, alikwenda kumwangalia mtoto huyo kama alipelekwa hospitalini. Alipofika nyumbani kwa Debora, alimkuta mtoto huyo akiwa katika hali mbaya na hakupelekwa hospitalini.

Shahidi huyo alidai kuwa Aprili 4, mwaka huu, alikwenda Kituo cha Polisi Nyarugusu kutoa taarifa na polisi walimwambia aende akamchukuwe mtoto huyo, ndipo alikwenda nyumbani kwa Debora na kumchukua mtoto huyo, akampeleka Kituo cha Polisi Nyarugusu ambako alipewa Fomu Na. 3 ya Polisi (PF3) kisha kumpeleka mtoto huyo Kituo cha Afya Nyarugusu.

Shahidi huyo alidai kuwa alipofika Kituo cha Afya Nyarugusu walikataa kumpokea mtoto huyo kutokana na hali yake kuwa mbaya, hivyo alimpeleka katika Hospitali ya Wilaya ya Geita ambako alipokewa na kulazwa kwa ajili ya matibabu.

Alidai kuwa Aprili 17, 2023, mtoto huyo alipatiwa rukhsa ya kutoka hospitalini na kupelekwa nyumbani kwa bibi yake (bibi wa mtoto) ambaye alikubali kukaa na mtoto huyo kwa kuwa nyumbani kwa baba yake alikuwa anaishi na mama wa kambo.

Shahidi wa pili wa Upande wa Jamhuri ni Debora Abdallah (31) - mama mdogo wa mtoto huyo. Akiongozwa na Wakili wa Serikali Venance Mkonongo, alidai kuwa Aprili 3, 2023, saa 12 jioni, wakati akitoka kanisani, alimkuta mtoto huyo nyumbani kwake akiwa analia na amechomwa viganja vya mikono yote miwili na alipomwuliza mhusika wa ukatili huo, alidai ni baba yake mzazi - Daudi.

Debora alidai alimwuliza mwanawe huyo sababu za baba yake kumchoma kwa maji ya moto, mtoto huyo alidai aliokota Sh 5,000 na kumpelekea baba yake mzazi, Daudi na baada ya kukabidhi noti hiyo kwa baba yake, alifika nyumbani kwao mtu ambaye alikuwa amepoteza fedha, ndipo baba yake aliingia jikoni na kuchukua maji ya moto na kumchoma mtoto wake viganja vya mikono.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya mtoto huyo kumweleza kilichotokea, alikwenda hadi nyumbani kwa shemeji yake aitwaye Mathias Daudi na alipofika alimwuliza kama kweli ni yeye aliyemwunguza mtoto. Alidai alijibu 'ndiyo lakini nimeghafirika tu, nikamchoma mikono kwa kumwagia maji ya moto'.

Alidai kuwa Aprili 4, 2023, Ofisa Ustawi wa Jamii Kata ya Nyarugusu, alifika nyumbani kwake na kumwomba amchukuwe mtoto kwa madai kuwa anampeleka hospitalini. Akampatia.

"Nilimpatia mtoto na akaondoka naye na ilipofika Aprili 17, 2023, mtoto huyo alipelekwa kwa bibi yake akiwa amepona majeraha yake ya mikononi," alidai.

Baada ya shahidi huyo kumaliza kutoa ushahidi wake, Hakimu Mkazi Mwandamizi Kijuwile alimwuliza mshtakiwa kama alikuwa na maswali ya kumwuliza shahidi huyo. Mshtakiwa huyo alidai kuwa na maswali kama ifuatavyo:

**Mshtakiwa:** Shahidi ulimkuta mtoto ameishapata matibabu?

**Shahidi:** Hapana.

**Mshtakiwa:** Shahidi ulinikuta nimeishachukua PF3?

**Shahidi:** Hiyo PF3 mimi siijui.

**Mshtakiwa:** Unaamini vipi kama mtoto nimemchoma mimi kwa maji ya moto?

**Shahidi:** Wewe mwenyewe ndiye uliyeniambia kuwa umemchoma mtoto wako kwa maji ya moto kwenye viganja vya mikono yote miwili.

Baada ya mshtakiwa kumaliza kumwuliza maswali shahidi wa pili wa upande wa Jamhuri, Wakili wa Serikali Mkonongo alidai kuwa kwa siku hiyo alikuwa na mashahidi wawili na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliobaki.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Kijuwile alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Agosti 28 mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kuwasikiliza mashahidi wengine waliyobaki.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Mkonongo alidai mahakamani kuwa Aprili Mosi mwaka huu, maeneo ya Nyarugusu, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimwunguza mtoto wake msichana mwenye umri wa miaka tisa kwa kumwagia maji ya moto katika viganja vya mikono yote miwili na kumsababishia maumivu makali mwilini mwake. Kitendo hicho ni kinyume cha sheria.

# Watumishi halmashauri mbaroni tuhuma uhujumu Mfuko wa Jimbo

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita inarajia kuwafikisha mahakamani watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Geita kwa tuhuma za kuhujumu fedha za Mfuko wa Jimbo la Geita Mjini.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Leonidas Felix, aliwataja watuhumiwa hao ni Dorini Mushi ambaye ni Ofisa Ugavi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Salima Amri - Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Butundwe na Joseph Lefa - mzabuni wote kwa pamoja wanadaiwa kuhujumu fedha za Mfuko wa Jimbo la Geita Mjini.

Felix alidai kuwa kwa njia za udanganyifu, walidai kwamba walipeleka matofali 3,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Nyakagwe huku wakijua wamepeleka matofali 1,973, hivyo walikuwa na nia ovu.

Alisema kuwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu, TAKUKURU imefuatilia utekelezaji wa wa miradi ya maendeleo 33 yenye thamani ya Sh. bilioni 16.8 inayotekelezwa katika sekta za elimu, afya, miundombinu ya barabara, utawala na maji.

Alisema kati ya miradi hiyo iliyofuatiliwa utekelezaji wake, miradi 12 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.6 ilibainika kuwa na upungufu na viashiria vya rushwa na hatua zilichukuliwa.

Felix pia alisema elimu ilitolewa kwa watendaji juu ya usimamizi wa matumizi ya fedha na uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi katika matumizi ya fedha za elimu bila malipo kwa kumshirikisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio unaendelea.

Alisema halmashauri pamoja na wanufaika wa mikopo pia wamepewa elimu ya matumizi sahihi ya mikopo kwa kuzingatia sheria na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio unaendelea.

Alisema wasiokuwa na leseni za biashara wamepigwa faini na kutakiwa kukata leseni na wamiliki wa nyumba za kulala wageni maelekezo yalitolewa kwa kufuata taratibu na sheria za uendeshaji wa biashara husika.

Felix alisema katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu, walipokea malalamiko 51 na yaliyohusu rushwa ni 41 na uchunguzi wake umeanza. Malalamiko yasiyohusu rushwa ni 10 na malalamiko ambayo uchunguzi wake umekamilika ni sita. Yameombewa vibali vya mashtaka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na malalamiko manne yamerudi na kibali cha mashtaka.

Alisema malalamiko 35 yanaendelea na uchunguzi, kesi mpya sita zilifunguliwa, kesi zinazoendelea mahakamani ni 10 na kesi walizoshinda ni tatu.



# Wananchi wazima jaribio la binti kutoa ujauzito

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KAMATI ya wananchi wa Kata ya Kahe Magharibi, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, inayopambana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto imefanikiwa kuzima jaribio la msichana mwenye umri wa miaka 17 kutaka kumshawishi daktari amsaidie kuutoa ujauzito alionao.

Mshichana huyo (jina limehifadhiwa) alikwenda katika Kituo cha Afya Kahe, akitaka kuitoa mimba hiyo baada ya kudai kukata tamaa kutokana na mwanaume aliyempa ujauzito kumsaliti na kisha kumkana.

Akizungumzia jaribio hilo, Katibu wa Kamati ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), ambaye ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Kahe Magharibi, Ruth Arega, alisema yeye na wenzake, wamefanikiwa kukaa na mtoto huyo na kumjenga kisaikolojia na kisha kukubali kuachana na mpango huo.

Kamati hiyo imepata mafanikio hayo baada ya kupatiwa mafunzo maalum na Shirika la Kiraia la TUSONGE CDO, linalotekeleza Mradi wa Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, chini ya ufadhili wa Shirika la The Foundation For Civil Society.

"Mtoto huyu aliona kama amefikia mwisho wa maisha yake, akawa mnyonge sana na mwanaume aliyempa ujauzito hakuwa tayari kumtunza msichana na kutunza ule ujauzito.

Baada ya kufikiri sana akaamua kwenda kituo cha afya, akiomba msaada atoe ujauzito alionao. Bahati nzuri pale tuna mjumbe wa MTAKUWWA, ambaye ni muuguzi, akatushirikisha jambo hilo na tukashirikiana nae kumpa elimu ya ushauri na kusitisha uamuzi wake".

Jonas Mlay, Mkazi wa Kijiji cha Ngaseni na Katibu wa dawati la kupinga ukatili Kata ya Kahe Magharibi, alisema moja ya mafanikio waliyoyapata kutokana na mradi wa kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ni mwanaume aliyeigomea Kamati ya MTAKUWWA kufungwa kifungo cha miezi sita jela na kuamriwa kulipa Sh.80,000 kila mwezi baada ya kumaliza adhabu hiyo.

Mwanaume huyo, alimtelekeza mke wake na watoto wawili na kuacha kuhudumia matunzo.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Monica Kikwati, akielezea changamoto za mapambano ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kupitia mradi huo, alisema tatizo kubwa la wakazi wa Kahe Magharibi ni uelewa mdogo kuhusu ukatili wa kijinsia na wengi wao wanapofanyiwa vitendo hivyo, hawako tayari kuviweka wazi ili kupata msaada.

Mratibu wa mradi huo wa Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kutoka Shirika la TUSONGE CDO, Eva Minja, alisema kamati hiyo baada ya kujengewa uwezo imepewa jukumu la kufuatilia na kupambana na vitendo hivyo katika Kata ya Kahe Magharibi.



Mratibu wa Elimu Kata ya Masuguru wilayani Muheza mkoani Tanga, Njingo Buzuka (kushoto), akimsaidia mtoto kufunga mkanda wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Muheza katika kata ya Masuguru, alimpongeza Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Benard Luanda, kwa kusimamia ukarabati wa madarasa kwa fedha za jimbo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TSB yajipanga kuzalisha tani 60,000 za mkonge

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKURUGENZI Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona, amesema kuwa moja ya malengo ya bodi hiyo kwa mwaka huu 2023 ni kuzalisha tani 60,000 kutoka tani 48,000 mwaka 2022.

Kambona alisema mwaka 2020 wakati TSB inapewa jukumu na serikali la kuhakikisha uzalishaji unapanda hadi kufikia tani 120,000 mwaka 2025, ilikuwa inazalisha tani 36,000 kwa mwaka na sasa hivi wamefunga mwaka 2022 kwa kuzalisha tani 48,000.

"Lengo letu ni kufikisha tani 60,000 na tayari hadi kufikia Juni mwaka huu tulikuwa tumeshazalisha tani 34,000. Kwa hiyo tunajiona kabisa tutamaliza mwaka 2023 kwa kuzalisha tani 60,000 bila wasiwasi. "Jitihada zimeshafanyika ambapo serikali imeongeza bajeti ya maendeleo ya Bodi ya Mkonge kwa kuiwezesha kupata vyombo vya usafiri kwa ajili ya kushughulikia upatikanaji wa takwimu ambao ulikuwa kikwazo,

"Na ndiyo maana utaona sasa hivi takwimu zimepanda siyo kwamba mkonge haukuwepo lakini takwimu zilikuwa hazikusanywi ipasavyo, kimsingi mabadiliko ni makubwa sana," alisema.

Akizungumzia takwimu za mapato Kambona alifafanua kwamba tangu serikali imechukua juhudi za kufufua mkonge mwaka 2019 na kutambulishwa kuwa zao la kimkakati, mauzo ya nje yameongezeka ambapo pekee yamefikia Dola za Marekani milioni 56 kutoka Dola milioni 42 kwa kipindi cha miaka miwili.

"Lakini mauzo ya ndani pia yaliongezeka kutoka Sh. bilioni 41 hadi sasa Sh. bilioni 43 kwa soko la ndani, kwa hiyo soko la nje limefanya vizuri zaidi yaani mkonge mwingi umeuzwa zaidi nje kuliko ndani lakini mwisho wa siku takwimu zimepanda," alisema.

Pia alibainisha kwamba pamoja na hayo wastani wa mauzo ya singa za mkonge tani moja ni Sh. milioni 3.5 kwa madaraja ya juu.

# DC awapa somo walimu mikopo kausha damu

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKUU wa Wilaya ya Tanga, James Kaji, amewataka walimu mkoani humo kuacha kujiingiza kwenye mikopo kandamizi ambayo imekuwa ikiwapa wakati mgumu.

Amesema hatua hiyo inawasababisha kushindwa kutimiza wajibu wao wa kufundisha kutokana na kutumia muda mwingi kufikiria namna ya kuirejesha.

Badala yake amewataka kuhakikisha wanaitumia Benki ya NMB kutokana na bidhaa zao wanazotoa za mikopo ambazo zimeweza kuwainua kimapato na hatimaye kuwakwamua kiuchumi badala ya kujiingiza kwenye mikopo kandamizi.

Kaji aliyasema hayo juzi wakati alipomwakilisha Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema katika kongamano la siku ya walimu wa Mkoa wa Tanga lililoandaliwa na Benki ya NMB.

Ambapo alisema kwamba hilo ni kutokana na kwamba benki hiyo kusheheni huduma mbalimbali ambazo wanaweza kuzitumia katikaa kujikwamua kiuchumi na kuondokana na mikopo kandamizi.

Alisema: "Niwapongeza NMB kwa kuandaa kongamano hili kwa walimu ni ya kipekee kwani imetoa msisitizo kwa kutumia nguvu nyingi kuwezesha walimu kwenye shule za msingi na sekondari kwani wamekuwa wakiishi kwenye mazingira magumu kutokana na kujiuingiza kwenye mikopo umiza," alisema. Aidha, alisema mikopo hiyo imekuwa ikiwaumiza na hivyo kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kuweza kufundisha kutokana na kutumia muda mwingi kufikiria namna ya kuirejesha.

"Warsha hii imekuja wakati muafaka na niipongeza NMB nitoa wito kwa walimu kuweza kutumia NMB kutokana na bidhaa zao wanazotoa za mikopo ambapo lakini tumeshuhudia jinsi benki ilivyoweza kuwainua kimapato na kuweza kuboresha maisha yao hali inayoongeza uwezo kwenye utumishi wa kazi zao za kila siku," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Bima wa Benki ya NMB, Martin Massawe alisema kwamba wamezindua mpango maalumu kwa ajili ya walimu ambao waliuita "Specho" na wamekuja Tanga kutoa elimu zaidi na kusisitiza juu ya huo mpango unaomwezesha mwalimu kupata mikopo yenye riba nafuu ikiwemo ya kujiendeleza kielimu wao na watoto wao.

Alisema pia wanatoa mikopo ya biashara ndogo, ujenzi, vyombo vya moto kama bodaboda na pikipiki za miguu mitatu ikiwemo kupata mkopo wa bima ambayo inawezesha walimu kulipa bima kujikinga na majanga mbalimbali.

"Lakini pia tunatoa mikopo ya pembejeo na mashine za kilimo fursa za kushiriki promosheni na kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo elimu ya kifedha kwa walimu na kadhalika," alisema.

Hata hivyo alisema kwamba utafiti unaonyesha kati ya Watanzania milioni 60 ni asilimia 22 tu ndio wenye akaunti za benki pia zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanaamiliki simu za mkononi na wana uwezo wa kufanya malipo na miamala kupitia simu zao za mkononi.

Hata hivyo alisema hivi karibuni wamezindua huduma kubwa tatu ambazo zinaendelea kuleta mapinduzi makubwa katika sekta hya kibenki Tanzania ambazo ni mikopo kidigitali, NMB Pesa Wakala na NMB Lipa Mkononi.

Alisemna kupitia mifumo hiyo wameweza kuwafikia Watanzania wengi zaidi na hivyo kuchangia kuongeza idadi ya wanaotumia huduma za kibenki na pia hata kuwasaidia walimu ambao wanaweza wakawa mbali na matawi ya benki.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Ladislaus Baraka alisema siku ya mwalimu kwa Benki ya NMB ilianzia Mkoa wa Tanga miaka ya nyuma Wilaya ya Korogwe kwa zaidi ya miaka saba iliyopita na wameendelea kuboresha huduma zao.



# Wenye ualbino wapewa mafunzo ya kareti wajilinde

**Na Neema Charles,** SAUT

VIJANA wenye ulemavu wa ngozi 240 kutoka mikoa mbalimbali wamepatiwa mafunzo ya kareti kwa ajili ya kujihami na kujilinda na uvamizi wa watu wasiokuwa na nia njema kwao.

Hatua hiyo itawasaidia kujiamini wakati wote wanapokuwa katika mazingira ya nyumbani hata masomoni.

Wakizungumza baada ya mafunzo hayo yaliyodhaminiwa na Shirika la Under The Same Sun (UTSS) kwa siku saba walisema mafunzo hayo yatawasaidia kujilinda katika kipindi chote cha maisha yao.

Maneno Lukas mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma alisema mafunzo waliyopatiwa yamekuwa muhimu katika kuhakikisha wanajilinda, kuwa watii na wenye nidhamu kwa wakati wote katika maisha.

Naye Daniel Maduya mwanafunzi wa kidato cha sita alisema: "Licha ya mafunzo haya ya kareti kumefunzwa pia maarifa ya jamii, ujasiriamali, uchaguzi ya taaluma, kazi pamoja na namna ya kutafuta kazi na kufanya usaili kwa ufanisi ili tuweze kupata ajira na kuwa wafanyakazi bora na sio kuonewa huruma katika kupatiwa ajira."

Diana Bonephace, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) alieleza kuwa mafunzo hayo yameendelea kuwaimarisha na kuwapa nguvu za kujihami wakati wote wanapokuwa katika shughuli zao za kila siku.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu Tanzania, Alfred Kapole, alisema kuwa mafunzo ya namna hiyo yanatakiwa kuwa endelevu kwa vijana hao pamoja na wengine ambao hawajapata nafasi ya kujiunga katika ufadhili huo.

Aliiomba serikali pamoja na wadau mbalimbali kuweka mfumo rafiki utakaowawezesha vijana wenye ualbino kupata nafasi ya kukutana na kubadilisha mawazo na fursa mbalimbali zilizopo.

"Vijana hawa wana uwezo wa kikazi na wanaajirika lakini kuna umuhimu wa elimu kuendelea kutolewa kwa waajiri ambao bado wana imani kuwa watu wenye ualbino ni mzigo kazini ili waweze kuwapa fursa za ajira," alisema.

Mfadhili wa vijana hao kutoka UTTS, Peter Ash aliwataka vijana hao kuhakikisha wanakuwa na nidhamu wakati wote wawapo katika shughuli na masomo yao huku wakizitumikia vyema nguzo za shirika hilo ikiwa ni pamoja na kuwa na imani katika dini.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla (katikati), akipokea zawadi kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo (TIB), Lilian Mbassy (kulia), baada ya kufungua mkutano wa wadau wa benki hiyo jijini Mwanza. Kushoto ni Meneja wa benki Kanda ya Mwanza, Widson Swalala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji madini waomba elimu ya kujikinga na majanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika machimbo ya Ntambalale wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba serikali pamoja na wadau kutoa mafunzo ya kujilinda na majanga katika maeneo yao.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakati Taasisi ya Kuendeleza Wachimbaji wadogo wa Madini nchini (FADev) lilipotoa msaada wa vifaa vya kujikinga dhidi ya majanga wanapokuwa mgodini. Mmoja wa wachimbaji hao wadogo, Anthony Thomas, alisema wachimbaji wengi hawana elimu ya usalama wao na wamekuwa wakifanya shughuli hizo kimazoea na hupata madhara ya mara kwa mara kutokana na kutovaa vifaa kinga.

"Vifaa kinga ni muhimu sana katika shughuli zetu hizi za uchimbaji madini, ukiangalia mikono yangu nimejibonda sana na hata chembechembe za miamba huingia kwenye macho yetu, tunashukuru kupata elimu ya usalama na vifaa kinga," alisema Thomas.

Mwenyekiti wa Isanja Ndugu Gold Mine, Hamis Mabubu, alisema upatikanaji wa elimu pamoja na vifaa kinga vitasaidia kuwakinga walichimbaji hao katika shughuli za uchimbaji salama.

"Vifaa hivi vitatumika kwa madhumuni yaliyotarajiwa na vikichakaa watanunua vingine kwa ajili ya kuwalinda wachimbaji sababu wameshapata elimu ya afya na usalama kazini," alisema. Katibu Mtendaji wa taasisi hiyo, Mhandisi Theonistina Mwasha, alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini juu ya kuzingatia fya na usalama wao kazini, hivyo wakaona ni vyema kuwapatia na vifaa kinga ambavyo vitawakinga na madhara mbalimbali katika uchimbaji huo wa madini.

"Vifaa kinga ambavyo tumevitoa ni viatu vya usalama, kofia ngumu, maski, miwano, gloves, koti za kuakisi mwanga hasa wanapokuwa chini ya mashimo na vifaa vya kuziba masikio," alisema Mhandisi Mwasha.

# Meya akagua miradi, atoa maagizo kwa wasimamizi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MSTAHIKI Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Sima Constantine, amefanya ukaguzi wa miradi ya elimu inayotekelezwa katika Jiji hilo na kuwataka wasimamizi wa miradi hiyo kusimamia kikamilifu ili iweze kutoa huduma kama ilivyotarajiwa.

Sima alikagua miradi ya miwili ya Boost ambayo ni Shule ya Msingi Kanenwa ujenzi wake ukiwa umefikia asilimia 90 na Shule ya Msingi Ng'wanghalanga pia utekelezaji wake umefikia asilimia 96 yote ikiwa na thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 1.8.

Alisema miradi hiyo imelenga kuondoa adha ya watoto kutembea umbali mrefu na kuwapa nafasi ya kusoma katika mazingira mazuri lengo likiwa ni kupata wanafunzi wenye uwezo mzuri kielimu.

"Na miradi yote ambayo haijakamilika niwaombe hakikisheni inakamilika kwa wakati ili ianze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa ili kiwango cha elimu kiendelee kuinuka siku hadi siku," alisisitiza.

Vilevile alitembelea na kukagua ujenzi wa miundombinu katika Shule ya Nsumba ambayo ni bweni moja, vyumba vinne vya madarasa na matundu ya vyoo vyote vikigharimu zaidi ya Sh. milioni 240 na kuonesha kufurahishwa na kuendelea kupanda kwa kiwango cha ufaulu katika shule hiyo ya kidato cha tano na sita.

Inaelezwa kuwa katika mwaka wa masomo 2023 shule hiyo imepata wastani wa juu zaidi wa alama ya jumla (GPA) ya 2.4 ambayo haijawahi kufikiwa na shule hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1952 huku wanafunzi wenye ufaulu wa daraja la kwanza wakiwa 264.

Akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa mbele ya Mstahiki Meya, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Nsumba, Denis Mwakisimba, alieleza kuwa ongezeko la ufaulu katika shule hiyo limesababishwa na uwepo wa miundombinu ya kutosha sambamba na walimu kufanya kazi katika mazingira rafiki.

Alisema mwaka huu imefaulisha wanafunzi kwa daraja la kwanza 264 daraja la pili 141, daraja la tatu 23 ikiwa haina daraja la nne wala sifuri, kwamba kati ya shule zote zilizopo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza shule hiyo imeendelea kushika nafasi ya kwanza kwa miaka miwili.

Alisema: "Haya ni matunda ya fedha ambazo tumeendelea kupatiwa na Rais Samia Suluhu Hassani ikiwa ni pamoja na hizi Sh.milioni 800 za ujenzi wa miundombinu pamoja na walimu kupandishwa madaraja na kufanya kazi kwa kujituma.

Nipashe **Spotiko**




VIUNGO WAKABAJI WA5 BORA ZAIDI DUNIANI KWA HIVI SASA UK. 12-13



# WACHEZAJI 3 WANAOWEZA KUZIBA PENGO LA DEMBELE

DEMBELE

**BARCELONA,** Hispania

BAADA ya ripoti ya Fabrizio Romano kumhusisha Ousmane Dembele na Paris Saint-Germain, wababe hao wa Ufaransa walifanikisha rasmi usajili wake kwa ada ya euro milioni 50 kutoka Barcelona msimu huu wa joto.

Agosti 12, 2023, Dembele alitangazwa rasmi kurudi Ufaransa na kujiunga na mabingwa mara 10 wa Ligi Kuu nchini humo Paris Saint-Germain kuelekea msimu wa 2023-24.

Dembele mwenye umri wa miaka 26 amekuwa mmoja wa mawinga wenye uwezo na angavu zaidi wa Barcelona katika nyakati za kisasa, licha ya mzozo wake usioisha na utimamu wake wa mwili.

Dembele anafahamika zaidi kwa kasi na ustadi wake wa kuwapiga chenga walinzi mfululizo.

Dembele alifunga mabao 40 na kutoa asisti 43 katika michezo 185 kwa upande wa wababe hao wa Hispania. Kadhalika ana uwezo wa kukimbia na mpira kutoka pembeni hadi kwenye sanduku la penalti la mpinzani.

Wakati wowote anapokuwa katika kiwango bora zaidi uwanjani, Dembele anakuwa mgumu kuzuilika.

Anajua jinsi ya kumhadaa mpinzani wake na hii inamruhusu kuchukua fursa ya makosa ya wapinzani kuweza kuwaadhibu kwa mabao.

Makala haya inawaangalia wachezaji watatu ambao wanaweza kuchukua nafasi ya Dembele pale Barcelona baada ya yeye kuondoka.

### #3 Joao Felix (Manchester United)

Mchezaji ambaye ameonyesha hadharani nia yake ya kujiunga na Barcelona ni Joao Felix.

Ni mshambuliaji bora ambaye mtazamo na uamuzi wake katika shambulio ni wa kushangaza. Vile vile, uwezo wake wa kumaliza ni wa ajabu. Wakati msimu wa 2022-23 ulikuwa mgumu kwa chipukizi huyo, alifunga mabao manne katika mechi 20 kwenye kipindi chake cha mkopo akiwa Chelsea.

Hata hivyo, baada ya kusajili michango 52 ya mabao kwa Atletico Madrid, Diego Simeone, anaweza kusita kumuuza ikiwa pendekezo hilo si la mdomoni pekee. Hii inaweza kusimama kama kizuizi kikubwa katika mpango huu.

### #2 Kingsley Coman (Bayern Munich)

Kumbadilisha Mfaransa na kuchukua mshirika mwenzake huenda lisiwe wazo baya, Coman ni mmoja wa walengwa kwenye orodha ya Barcelona. Nyota huyo anajulikana sana kwa umahiri wake na ubunifu katika kushambulia.

Coman amefunga mabao 58 na kusajili mabao 63 katika mechi 267 alizoichezea Bayern Munich.

Hatimaye, baada ya kucheza pamoja hapo awali na Robert Lewandowski, wawili hao wanaweza kufanya kazi tena pamoja kwa ufanisi kule Camp Nou.

### #1 Bernardo Silva (Manchester City)

Unapozungumzia washambuliaji hodari na wenye tija, mmoja wa wahusika wanaokuja akilini ni Bernardo Silva. Fowadi huyo wa Ureno ana nguvu na uwezo wake wa kushambulia ni wa kustaajabisha.

Kinachomfanya aonekane bora zaidi ni uelekevu wake pamoja na hekima yake katika theluthi ya mwisho ya uwanja. Ingawa hakuna shaka kusajiliwa kwake kutaboresha safu ya ushambuliaji ya Barcelona, Manchester City wanaweza kulazimika kutaka fedha nyingi ikiwa watamruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kuondoka katika klabu hiyo.

Kwa mujibu wa Barca Times, Silva amekuwa akihusishwa na Barcelona, na kuna tetesi anatamani kujiunga na timu hiyo ya Hispania.

Silva amefunga mabao 55 na kutoa asisti 59 katika michezo 306 aliyoichezea Manchester City. Itakuwa ya kuvutia kuona kama atajiunga na wababe hao wa Katalunya msimu huu wa joto.

## ISIKUPITE

Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao katika msimu mpya wa Ligi Kuu England ulioanza Ijumaa iliyopita wakati timu yake ikipata ushindi wa ugenini wa magoli 3-0 dhidi ya Burnley.



# VIUNGO WAKABAJI WATANO BORA ZAIDI DUNIANI KWA HIVI SASA



CASEMIRO

**LONDON,** England

VIUNGO wakabaji au walinzi mara nyingi ndio mashujaa wasiojulikana wa timu yoyote ya soka yenye mafanikio. Wanachukua jukumu muhimu katika mchezo mzuri wa mpira wa miguu, kulinda na kuanzisha mashambulizi kutoka kwenye nafasi za kina.

**Viungo wa ulinzi wanajiweka mbele kidogo ya safu ya ulinzi na jukumu lao kuu ni kuzuia au kuvunja mashambulizi ya wapinzani. Kukaba kwa nguvu, akili ya mchezo na ufahamu wa nafasi na sifa zinazohitajika.**

Zaidi ya hayo, viungo wa ulinzi mara nyingi hufanya kama vifaa vya kuzindua mashambulizi. Zaidi ya kuvunja mchezo, viungo wa ulinzi husaidia kubadilisha kasi kwa upande wa timu yao kwa kusambaza mpira kwa usahihi kwa wenzao wa juu zaidi.

Viungo wa ulinzi au wakabaki wa kati huamuru presha ya mchezo, kudhibiti vita vya kati na kujaribu kupata faida kwa upande wao katikati ya uwanja.

Hapa tunawatazama viungo wakabaji bora zaidi katika soka la dunia ya hivi sasa.

## #5 AURELIEN TCHOUAMENI (REAL MADRID)

Aurelien Tchouameni alihamia Real Madrid kutoka AS Monaco msimu wa joto wa mwaka 2022. Los Blancos hao walikuwa wakimfuatilia kwa muda mrefu na ulikuwa ni wakati wa kuanza mchakato wa kurekebisha muundo wao.

Tchouameni ni mkabaji mgumu na mharibifu wa safu ya kati. Mchezaji huyo wa zamani wa AS Monaco pia ni mkali na msomaji mzuri wa mchezo huo. Tchouameni ni hodari wa kuingilia kati na kuwa tishio kabisa katikati ya uwanja kwa upande wa timu pinzani. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 pia amethibitika ni nadhifu katika kumiliki mpira.

Atahitaji kufanya makubwa zaidi ili kuthibitisha thamani yake ya euro milioni 80 alizonunuliwa. Ishara za mapema zimekuwa nzuri. Mfaransa huyo alifanya kazi nzuri kwenye safu ya kiungo ya Real Madrid msimu uliopita licha ya kupewa kazi kubwa ya kuchukua jukumu la Casemiro aliyeondoka.

## #4 DECLAN RICE (ARSENAL)

Ukweli wachezaji kama Aurelien Tchouameni na Declan Rice walisajiliwa kwa ada kubwa za uhamisho ni uthibitisho tosha wa jinsi viungo wa ulinzi wamekuwa muhimu katika mchezo wa kisasa. Rice alijiunga na Arsenal kutoka West Ham msimu huu kwa kitita cha euro milioni 116.

Raia huyo wa Uingereza ana uwezo mkubwa wa kusoma mchezo, sio tu ni bora katika kuvunja mashambulizi lakini katika kuendeleza mpira na hata kutengeneza nafasi kwa upande wa timu yake. Sasa kwa kuwa Rice amejiunga na Arsenal, ni wakati wa kupeleka mchezo wake kwenye kiwango cha juu na kuongeza uwezo wake.

## #3 CASEMIRO (MANCHESTER UNITED)

Mshindi mara tano wa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Casemiro alihamia Manchester United ili kutoa nafasi kwa wachezaji wachanga kwenye kikosi cha Real Madrid. Hata hivyo, hiyo haimaanishi ubora wake ulikuwa umeshuka au miaka yake bora ilikuwa nyuma yake.

Mbrazil huyo alikuwa sehemu muhimu ya kikosi cha kwanza cha Manchester United katika kipindi cha kampeni yake ya kwanza nchini England. Aliongeza chuma kwenye safu ya kiungo ya United na huku yeye akilinda safu ya ulinzi.

Sio tu Casemiro amekuwa mzuri katika kuvunja mchezo na kuonyesha ujuzi wake kama mharibifu wa safu ya kati, lakini pia amekuwa bora kwenye kufunga. Alifunga mabao saba na kutoa pasi saba za mabao kwa Mashetani Wekundu hao kwenye mechi 53 katika mashindano yote msimu uliopita.

## #2 JOSHUA KIMMICH (BAYERN MUNICH)

Joshua Kimmich ndiye moyo wa Bayern Munich. Mpiganaji mshindani na shupavu wa kiungo, Kimmich ni mmoja wa viungo bora wa kizazi chake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani pia ni mmoja wa wachezaji wa kati wenye vipaji vya hali ya juu kwenye sayari hii hivi sasa.

Kwa sababu ya uwezo wake bora wa kusoma mchezo na ustadi wa ulinzi aliopata wakati wa siku zake za mwanzo kama beki wa kulia, Kimmich ni ukuta wa ulinzi kabisa peke yake. Zaidi ya hayo, ustadi wake wa uchezaji ni wa kiwango cha kimataifa.

## #1 RODRI (MANCHESTER CITY)

Rodri amekuwa mzuri kabisa kwa Manchester City kwenye safu ya kiungo. Ametoka msimu mmoja uliojaa mataji kwa klabu na nchi na amejidhihirisha ni kiungo mkabaji bora zaidi duniani.

Rodri ni mtu asiyechoka katika safu ya kiungo, anaweza kufanya kazi ya watu wawili katikati ya uwanja. Ukabaji wake ni mzuri na uwezo wake wa kukaba pasi ni wa kiwango cha juu pia. Rodri alifunga bao la ushindi kwa Man City katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Inter Milan msimu uliopita.

Alishinda taji la Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA akiwa na City msimu uliopita. Pia alishinda taji la Ligi ya Mataifa ya Uefa akiwa na Hispania msimu huu wa joto.

## Nukuu

"Nina furaha sasa kuwa sehemu ya wachezaji wa Bayern Munich. Bayern ni moja ya klabu kubwa duniani na kila siku nimekuwa nikisema ninahitaji kuendelea kushindana na kuthibitisha ubora wangu katika muda wote ninayocheza," **Harry Kane, ambaye atavaa jezi namba tisa alisema hayo baada ya kusaini mkataba mpya na Bayern utakaomweka klabuni hapo hadi mwaka 2027.**



"Sidhani kama tutakuwa bora kama msimu uliopita. Ni lazima kidogo. Tutajaribu kuizuia iwezekanavyo. Halafu, katika miezi minne, tutajaribu kufanya kile ambacho tumefanya kila msimu," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, alisema kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu England ulioanza Ijumaa iliyopita.**



"Udhamini huu utanufaisha ligi yetu ya Championship, Ligi ya vijana ya U-20 ambayo zamani ilikuwa inaitwa Uhai, sasa itapewa jina jipya kutoka kwa mdhamini wetu kwa sababu ana bidhaa nyingi na hatutaweza kutumia tena neno NBC, watatupa jina jingine na rasmi litakuwa linatumika hillo kwenye ligi hizi," **Wallace Karia, Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania akizungumza wakati wa kusaini mkataba mpya wa benchi hilo.**






Mabingwa watetezi Ligi Kuu Bara, Yanga'. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

# MECHI 10 KALI KUTAZAMWA LIGI KUU BARA 2023/2014

MSIMU mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unatarajiwa kuanza rasmi kesho kwa mechi tatu, Ihefu ikicheza dhidi ya Geita Gold kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbeya wakati Namungo itawakaribisha JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Majaliwa, mkoani Lindi na Coastal Union itakuwa mgeni wa Dodoma Jiji, Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

**Ligi hiyo itaendelea tena keshokutwa kwa Mashujaa FC ikiivaa Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma huku Azam Complex, Dar es Salaam wenyeji Azam watawakaribisha Tabora United.**

Simba itacheza mechi yake Agosti 17, mwaka huu dhidi ya Mtibwa Sugar na mabingwa watetezi, Yanga wataanza kampeni za kutetea taji Agosti 23, mwaka huu kwa kucheza dhidi ya KMC, Azam Complex.

Ukiachana na mechi hizo za raundi ya kwanza kuna mechi kati ambazo mashabiki wa soka nchini watakuwa na hamu nazo kutokana na ushindani na mvuto kwa sababu mbalimbali.

Mwandishi wa makala haya amekusanya mechi 10 ambazo zitavutia mashabiki wengi kwenda uwanjani au kuzitazama kupitia luninga.

**PRISONS vs SIMBA (Oktoba 3, 2023- Sokoine Mbeya)**

Mara nyingi mechi kati ya timu hizi mbili huwa ni ngumu, hasa zinapocheza Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

Simba imekuwa ikipata shida sana inapocheza dhidi ya Prisons kwenye uwanja huo na mara kadhaa hupoteza au sare ambazo humweka kwenye hali ngumu katika msimamo wa ligi. Pamoja na msimu uliopita Simba ilipata ushindi wa bao 1-0 likifungwa na Jonas Mkude ambaye kwa sasa hayupo kwenye kikosi hicho, bado mechi hii inatarajiwa kuwa ngumu.

**SINGIDA FG vs Simba- (TBA Liti, Singida)**

Bado mechi hii haijapangiwa tarehe rasmi, lakini ni moja kati ya pambano linalosubiriwa kwa hamu na mashabiki wengi wa soka nchini.

Singida Fountain Gate 'kutoa macho' zaidi inapocheza na Simba kama ilivyofanya kwenye Ngao ya Jamii na timu hizo kwenda hadi mikwaju ya penalti.

Itachezwa kwenye Uwanja wa CCM, Liti Singida ambako msimu uliopita timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, hivyo inatabiriwa haitokuwa mechi ya kitoto.

**YANGA vs AZAM (Oktoba 25, 2023- Mkapa)**

Siku hiyo kutakuwa patashika nguo kuchanika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga itakapopambana na Azam FC.

Kwa sasa inaonekana Azam kuwa mteja wa Yanga kwani imekuwa ikipoteza katika michuano mbalimbali, ikiwamo Ligi Kuu.

Kwa sasa ushindi mkubwa wa Azam kwa Yanga ni sare na tayari imeshafungwa kwenye Ngao ya Jamii, hivyo mashabiki watataka kuona kama uteja utaendelea au la.

**SIMBA vs YANGA- (TBA-Mkapa)**

Awali ikipangwa kucheza Novemba 5, 2023 lakini Bodi ya Ligi ikapata barua kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuiondoa Simba kwenye ratiba kuanzia Oktoba 20 hadi Novemba 21, mwaka huu kutokana itakuwa kwenye michuano ya African Football League.

Hata hivyo hii ni mechi inayosubiriwa kwa hamu zaidi kwani ndiyo 'dabi' kubwa na namba moja nchini Tanzania na inabeba hisia za mashabiki wa soka ndani na nje ya nchi.

**SIMBA vs AZAM (Novemba 28, 2023 Mkapa)**

Ni mechi ambayo mashabiki wanataka kuona kama Simba inaweza kujikwamua kwenye uteja kutoka kwa Azam FC.

Kwa misimu ya hivi karibuni Simba imekuwa haipindui kwa Azam, ikipoteza kila inapokutana nayo katika michuano mbalimbali, Ligi Kuu mpaka Kombe la FA.

Kwa usajili wa Simba uliofanyika msimu huu, wengi watataka kuona kama watazika uteja huo au wataendelea kuwa vibonde kwa Wanalambalamba.

**IHEFU vs PRISONS (Desemba 4, 2023 Highland Estates)**

Hii itakuwa ni 'dabi' ya Mbeya msimu huu, baada ya Mbeya City kushuka daraja.

Ihefu na Prisons zote ni timu za Mbeya, hivyo mashabiki wa soka, hasa wa jiji hilo watakuwa na hamu ya kuitazama 'dabi' yao itakayochezwa kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali.

**DODOMA JIJI vs SINGIDA FG (TBA Jamhuri)**

Mechi hii haijapangiwa tarehe kwa sababu Singida Fountain Gate itakuwa na majukumu ya kimataifa, ikicheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mashabiki wa soka, hususan wa Singida na Dodoma wanaisubiri kwa hamu mechi hii ambayo ni 'dabi' ya kanda ya kati na kuwa moja ya pambano litakalotazamwa sana.

**JKT TANZANIA vs MASHUJAA (Oktoba 20, 2023 Black Rhino)**

Oktoba 20 kutakuwa na mechi ambayo itazikutanisha timu ambazo za majeshi zilizopanda daraja msimu huu.

JKT Tanzania inayomilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), itapambana na wenzao kutoka Jeshi la Wananchi (JWTZ), Mashujaa FC katika mechi kali ya kutazamwa 'dabi' ya majeshi itakayochezwa Karatu, jijini Arusha.

**MASHUJAA vs TABORA UNITED (Desemba 3, 2023 -Lake Tanganyika)**

Desemba 3, mwaka huu kutakuwa na mechi ambayo itazikutanisha timu zilizopanda daraja msimu huu.

Tabora United na Mashujaa zote zimepanda daraja msimu huu na itakuwa ni mechi yao ya kwanza kukutana zikiwa Ligi Kuu, ingawa zimeshawahi kucheza wakati zipo Ligi ya Championship.

**IHEFU vs YANGA (Desemba 4, 2023- Highland Estates)**

Itakumbukwa msimu uliopita Yanga ilichafua rekodi yake ya kutofungwa mechi 50 ilipopoteza dhidi ya Ihefu kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali.

Ilicheza mechi 49 mfululizo bila kupoteza lakini ilipokwenda huko ikakutana na kipigo cha mabao 2-1.

Msimu huu mashabiki wa soka wanataka kuona kama Ihefu inaweza kufanya tena kwa kuifunga Yanga kama ilivyoifunga Novemba 29, mwaka jana.

**JE, WAJUA?**



Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, huenda akaondolewa moja kwa moja katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo endapo ataendelea na msimamo wake wa kukataa kuongeza mkataba mpya na vigogo hao wa Ligi Kuu Ufaransa. Mbappe anataka aondoke klabuni hapo kama mchezaji huru.



## HABARI DODOMA

# Wafanyakazi wengi ofisini wanakabiliwa uzito mkubwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TAKWIMU za Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa mwaka 2022/23, zinaonesha wafanyakazi 316,000 walipimwa afya kati yao asilimia 40 wanakabiliwa na uzito uliozidi.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye bonanza la Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) ambalo mgeni rasmi alikuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu, Majura Mahendeka kwa niaba ya Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka.

Alisema takwimu zilizokusanywa na OSHA katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini kwa mwaka huo, wafanyakazi 316,000 walipimwa afya na madaktari wa OSHA ambapo kati yao, wafanyakazi 126,400 sawa na asilimia 40 walikuwa na uzito uliozidi wastani na 15,800 sawa na asilimia tano walikuwa na shinikizo la juu la damu.

"Takwimu hizi ni kiashiria kuwa wafanyakazi wengi wapo katika hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza ambayo madhara yake hayaishii tu kwa mfanyakazi mwathirika bali hupelekea hasara kwa familia na taifa zima kwa ujumla kwa kupoteza nguvukazi," alisema Khadija. Alitoa rai kwa waajiri na wafanyakazi kuendelea kuzingatia ushauri ambao umekuwa ukitolewa na wataalamu wa OSHA baada ya kufanya ukaguzi na kuchunguza afya za wafanyakazi kwenye maeneo ya kazi ikiwamo kuanzisha programu za michezo mahali pa kazi.

Alisema OSHA imedhamini bonanza hilo ikiwa sehemu ya kampeni ya OSHA ya kuhamasisha uwapo wa programu za michezo kwenye maeneo ya kazi zinazolenga kushughulikia vihatarishi vya kisaikolojia kinachoyakumba maeneo mengi ya kazi duniani kote.

Akifungua bonanza hilo, Katibu Mkuu Mahendeka, alitoa wito kwa watumishi wa umma kubadili mtindo wa maisha kwa kujihusisha na michezo ili kulinda afya zao na hivyo kutoa mchango wao kikamilifu katika kuwahudumia wananchi.

Alisema: "Watumishi wa umma tutambue kwamba sisi ndio chachu ya maendeleo ya taifa kwakuwa ndio tunahusika na kupanga mipango yote ya maendeleo ya nchi pamoja na utekelezaji wake.

"Ili kutekeleza haya yote, watumishi wa umma hatuna budi kuwa na afya njema na akili timamu na mambo haya yanapatikana kupitia kuwa na mtindo bora wa maisha na mtindo bora wa maisha ni ule unaozingatia ulaji unaofaa, kufanya mazoezi na kuepuka matumizi ya vyakula na vinywaji vinavyoweza kuathiri afya."



Baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Maji na wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA) walipotembelea chanzo cha maji Mzakwe jijini Dodoma jana kuangalia uzalishaji wa huduma hiyo. **PICH: IBRAHIM JOSEPH**

# Watumishi afya wapewa jukumu kupunguza kero

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imewataka viongozi na watumishi wa sekta ya afya nchini kuwajibika kwenye majukumu yao ili kupunguza kero zinazojitokeza katika utoaji wa huduma.

Mkurugenzi wa Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Ntuli Kapologwe, alitoa kauli hiyo mjini hapa kwenye kikao cha majumuisho cha masuala ya kwa halmashauri saba za mkoa huo.

Alisema ni muhimu kuwapo na uwajibikaji ili kubaini mapungufu, kuboresha kwa kuweka mazingira bora ya upatikanaji kwa huduma ya afya kwa jamii. Mkurugenzi huyo alisema Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa katika kuwajali wananchi wake, kwa kuwajengea vituo vya afya, zahanati na hospitali na kuhakikisha kuna kuwapo na dawa, vifaa tiba na watumishi.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Kapologwe aliwaasa watumishi kufanya kazi kwa weledi na ushirikiano, ili kufanikisha kusudio la serikali.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, aliahidi kusimamia kwa dhati nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa halmashauri hiyo, ili kuhakikisha huduma za afya zinapatikana na kwa kiwango kilichokusudiwa.

# SIDO yawakumbusha wajasiriamali kuchangamkia mikopo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), limewataka wajasiriamali wadogo na wa kati kuchangamkia fursa ya mikopo ikiwamo inayotolewa na Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF).

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Prof. Sylvester Mpanduji, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu utekelezaji wa majukumu yao na mwelekeo wa mwaka 2023/24.

Alisema mfuko wa NEDF unatoa mikopo kwa kiwango cha juu cha Sh. milioni tano kwa riba ya asilimia tisa kwa miradi ya uzalishaji.

"Pia tumekuwa tukiwaunganisha katika Benki ya CRDB kupitia Wadhamani wa Mikopo wa Serikali (CGS). Jumla ya mikopo 5,006 yenye thamani ya Sh. bilioni 12.075 ilitolewa," alisema.

Alifafanua kuwa asilimia 45.3 ya mikopo ilitolewa kwa wanawake na asilimia 35 ilitolewa kwa miradi ya vijijini huku urejeshaji ni asilimia 91.

"Vile vile shirika limeunganisha wajasiriamali na Benki ya CRDB kupata mikopo ya kiwango cha hadi Sh. milioni 50, jumla ya mikopo 19 yenye thamani ya Sh. milioni 452 imetolewa," alisema.

Kadhalika, alisema kupitia karakana saba za SIDO mashine na vipuri 3,452 vilitengenezwa na kuuzwa kwa wajasiriamali.

Alisema katika awamu ya sita ya serikali shirika limewezesha kuanzishwa viwanda 678 vyenye ajira 2,686 mikoa yote na vinajishughulisha na uchakataji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu, uchomeleaji, useremala, ufumaji au useketaji.

Alibainisha shirika limejipanga kupanua wigo wa huduma kwa kufikia wananchi wengi kwenye ngazí za wilaya na kutoa huduma kupitia mafunzo mtandao.

# Mgogoro CWT, Baraza la Madiwani wachukua sura mpya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SAKATA la wanachama wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) dhidi ya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Karatu la kupokea na kuridhia kwa asilimia 100 ombi baadhi ya walimu kusitisha malipo ya makato ya ada za chama hicho katika mishahara yao limechukua sura mpya.

Rais wa Shirikisho la la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, jana alitoa tamko dhidi ya kitendo hicho alichokiita kuwa ni ukiukwaji wa sheria uliofanywa na kikao cha baraza hilo la madiwani.

"Leo tarehe 12 Agosti (juzi), 2023 TUCTA tumepokea taarifa kupitia wanachama wa CWT Halmashauri ya Wilaya ya Karatu wakionyesha kushangazwa na tukio la baraza la madiwani kupokea na kuridhia kwa asilimia 100 ombi la baadhi ya walimu kusitisha malipo ya makato ya ada za chama cha walimu toka katika mishahara yao na badala yake malipo hayo yalipwe chama walichokitambulisha kwa jina la Chama cha Kutetea na Kulinda Haki za Walimu Tanzania," alisema.

Alisema kitendo hicho cha baraza la madiwani siyo tu kimekiuka Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura ya 366 Marejeo ya Mwaka 2019, pia kimekinzana na utamaduni wa kiungwana na utawala bora wa mamlaka mbalimbali nchini kutoingilia taratibu na kanuni halali za mamlaka nyingine.

"TUCTA tunasema kitendo hiki kinastahili kukemewa kwa nguvu zote kwani sio jambo la kiugwana," alisema.

Alisema TUCTA kwa kauli moja wanapinga azimio la Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ya kukubali kwa kauli moja na kutekeleza maombi batili ya kusitishwa kwa malipo ya ada za uanachama wa baadhi ya walimu kwa Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

"Kupitia tamko hili TUCTA, tunaiomba serikali isifumbie macho jambo hili, wizara zenye dhamana ya serikali za wafanyakazi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu walikemee jambo hili na kuelekeza baraza la madiwani pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Karatu kusitisha mara moja azimio hilo na kuelekeza sheria izingatiwe katika masuala yote yanayohusu haki za wanachama na vyama vya wafanyakazi nchini," alisisitiza.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa taarifa walizopokea ambazo zimesambaa katika mitandao ya kijami kupitia video fupi inayoeleza tukio la kikao cha baraza la madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri, John Mahu alipokea na kuridhia kwa kauli moja maombi hayo.



## Bil.14.5/- zaongezwa kukamilisha mradi wa maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeongeza Sh. bilioni 14.5 kwenye ujenzi wa mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira ili ukamilike mapema na wananchi wa maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya waanze kunufaika.

Mkataba wa ujenzi wa mradi huo ulisainiwa Februari mwaka huu ambapo mkandarasi alilipwa Sh. bilioni 119 kama malipo ya awali.

Mkuregenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), CPA Gilbert Kayange, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anawasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji kwenye kikao cha Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema mkandarasi wa mradi huo alishaanza kazi na amefikia hatua nzuri na hivyo akauhakikishia uongozi wa Mkoa wa Mbeya kwamba watasimamia kwa umakini ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa muda.

"Mkandarasi alishapewa malipo ya awali lakini kwa sasa ameongezewa fedha ili kuongeza kasi zaidi, huu ni miongoni mwa miradi ya kimkakati ambayo sisi tunaisimamia," alisema Kayange.

Alisema mradi huo ukikamilika utakuwa ndio suluhisho la tatizo la maji katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya pamoja na maeneo ya wilaya zingine.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephene Mwakajumilo, aliagiza viongozi wa Mbeya-WSSA kumsimamia vizuri mkandarasi huyo ili atekeleze mradi huo kwa viwango vinavyostahili.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji na hivyo usimamizi unatakiwa kuwa wa kiwango kikubwa ili kusiwe na uhujumu.

# Serikali yaipiga 'stop' MUST kuongeza kozi kiholela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeuagiza uongozi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST) kuacha kuongeza kozi za fani zingine zisizohusiana na sayansi na teknolojia kwa maelezo kuwa wanaharibu lengo la uanzishwaji wake.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, alitoa angalizo hilo alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu mbalimbali chuoni hapo ambapo alisema chuo hicho kilianzishwa kwa ajili ya kuzalisha wataalamu wa sayansi na teknolojia.

Vilevile alisema chuo hicho kazi yake ni kufanya utafiti mbalimbali za kisayansi pamoja na kufundisha wanafunzi masuala ya sayansi na teknolojia kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema kitendo cha kuanzisha kozi zingine zikiwamo za uchumi kinaweza kikasababisha lengo la kuanzishwa kwake likapotea hasa endapo atatokea kiongozi ambaye anapendelea fani zisizokuwa za sayansi.

"Tukijidanganya kwamba tumekuwa imara sana kwenye sayansi na teknolojia, kilio kitatukuta muda sio mrefu, mimi sina uwezo wa kuingilia 'chapter' lakini kauli yangu ni kwamba acheni hizo fani zingine mwekeze zaidi kuzalisha wanasayansi," alisema Prof. Mkenda.

Alisema kwa Tanzania iliofikia inahitaji tafiti nyingi pamoja na kuzalisha wanasayansi wengi ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali na kulileta taifa maendeleo. Makamu Mkuu wa Chuo cha MUST, Prof. Aloyce Mvuma, alisema chuo hicho kimekuwa kikishirikiana na wadau mbalimbali kufanya utafiti za kisayansi ambazo zinalenga kutatua matatizo mbalimbali ya wananchi. Alisema kwa mwaka uliopita walizalisha zaidi ya machapisho 120 ambayo yalikuwa yanahusu masuala mbalimbali ya kimaendeleo na yanayohusu matatizo mbalimbali.

Alisema kwa mwaka huu wanaendelea na utafiti 17 ambazo wamefikia katika hatua mbalimbali na kwamba wanawashirikisha wadau mbalimbali wanaohusika kwenye shughuli husika.

Vilevile alisema wanafunzi wa chuo hicho pamoja na wafanyakazi wanashirikiana kutatua matatizo mbalimbali kwa kushirikiana na taasisi za serikali.

Alisema kwa sasa chuo hicho kinashirikiana na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kutatua kero ya matumizi ya maji kwa kuzalisha mita za malipo ya kabla (LUKU).

"Mita hizi ni za kisasa na ni za kidijitali ambazo zimebuniwa na wanafunzi wa chuo chetu wakishirikiana na wataalamu wetu, mpaka sasa zimeshafungwa mita 38 nchini kwa ajili ya majaribio," alisema Prof. Mvuma.

Alisema ubunifu huo umefanikiwa kutokana na ushirikiano walioupata kutoka RUWASA kwa maelezo kuwa fedha zinatolewa na wakala huo kwa ajili ya uzalishaji.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Carolyne Nombo, aliutaka uongozi wa chuo hicho kuwekeza nguvu kubwa kuwashawishi wanafunzi wa kike kujiunga na fani za sayansi.

Alisema uwiano kati ya wanaume na wanawake wanaosoma kwenye chuo hicho hauendani kutokana na idadi ya wanawake kuwa wachache.

Alisema chanzo cha uwiano huo ni wanawake kuogopa masomo ya sayansi wakiamini kwamba ni magumu hali ambayo inasababisha wasijiunge nayo.




Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Benki ya Azania, Augustino Matutu, akitoa maelezo kwa Rais Samia Suluhu Hassan alipotembelea banda la benki hiyo katika kilele cha maonesho ya Nanenane jijini Mbeya wiki iliyopita. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Esther Mang'enya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANAPA yaanza utekelezaji agizo la Waziri Mkuu

**Na Nebarty Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Usimamizi wa Hifadhi za Taifa (TANAPA), limeanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo ukanda wa Nyanda za Juu Kusini ili kuvutia watalii wengi kutembelea.

Agosti 3, mwaka huu akiwa kwenye maonyesho ya kimataifa ya wakulima (Nanenane), Waziri Mkuu Majaliwa alisema watalii wengi wanatembelea hifadhi zilizoko Ukanda wa Kaskazini pekee kutokana na kutokuwapo kwa usawa wa kutangaza.

Waziri Mkuu Majaliwa aliutaka uongozi wa TANAPA kutangaza vivutio vilivyopo ukanda huo wa Nyanda za Juu Kusini ili kupunguza msongamano wa watalii katika hifadhi ya kaskazini hasa Serengeti.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA, Kamishna wa Uhifadhi, William Mwakilema, alisema kwa sasa wameanza kuwekeza nguvu kutangaza vivutio vya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema hifadhi zilizoko ukanda huo ikiwamo Mikumi, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Udizungwa ni miongoni mwa hifadhi zinazonufaika na mradi wa uboreshaji wa mazingira ya utalii.

Alisema serikali ilipokea mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kuboresha miundombinu ndani ya hifadhi hizo pamoja na kupanua shughuli za uhifadhi.

Alisema miundombinu inayoboreshwa ndani ya hifadhi hizo ni barabara na viwanja vya ndege vilivyomo ndani ya hifadhi ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuvutia watalii.

"Tunaamini kwamba miundombinu hii itasaidia kuvutia watalii wengi kuja kutembelea hifadhi hizi zilizoko ukanda huu, lakini pia tutaendelea kutangaza kupitia njia mbalimbali ili zifahamike zaidi," alisema Kamishna Mwakilema.

Aidha alisema uwepo wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) ambao umewekewa miundombinu inayowezesha ndege za aina mbalimbali kutua ndani ya saa 24 ni kichocheo kingine cha utalii katika ukanda huo.

Alisema uwanja huo utasaidia watalii kufika kirahisi katika hifadhi za Kitulo, Ruaha na Katavi ambapo watakuwa wanakwenda kwenye maeneo hayo baada ya kutua kwenye uwanja huo.

Vilevile alisema vipo vivutio vingine ambavyo watalii wakifika kwenye uwanja huo wanaweza kuvifikia kikiwamo Kimondo kilichoko katika Kijiji cha Ndolezi Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe.

Pia alisema watatembelea misitu ya asili ya Mlima Rungwe, fukwe za Ziwa Nyasa zilizoko Kyela pamoja na Ziwa Ngozi lililopo wilayani Rungwe ambalo ni miongoni mwa maziwa ya kivolikano pamoja na kutembelea maporomoko ya maji ya Kalambo mkoani Rukwa.

Hata hivyo Mwakilema aliwataka Watanzania pia kutembelea vivutio vilivyopo kwenye maeneo yao ili kujifunza mambo mbalimbali yaliyomo.

Aliwataka pia kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa ajili ya kuwauzia watalii ili wajipatie kipato cha kuendeshea maisha yao.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ina vivutio mbalimbali vya asili zikiwamo tamaduni, hifadhi za taifa, milima na fukwe ambazo watalii wanaweza kutembelea na kujifunza.



# Mjumbe CCM ataja siri ufaulu wanafunzi kidato cha nne

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amesema kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa ya kidato cha nne Mkoa wa Kusini Unguja kumetokana na juhudi zinazochukuliwa na viongozi wa mkoa huo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Paje na Makunduchi katika mwendelezo wa ziara yake ya kukagua uhai wa chama mkoani humo.

Alisema kwa mwaka wa masomo 2022 Mkoa wa kusini Unguja umeongeza ufaulu kutokana na juhudi zilizochukuliwa na Jumuiya ya Mwanamke Initiative Foundation (MIF) kwa kushirikiana na Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM).

Mjumbe huyo ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alisema Serikali ya Zanzibar imefanya jitihada za kuanzisha masomo ya kidato cha tano na sita katika Shule ya Hasnuu Makame ili kupunguza umbali mrefu kwa wanafunzi kufuata elimu hiyo katika mkoa huo.

Aidha, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza zaidi ya Sh. bilioni 230 kwenye miradi mingi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa hospital za wilaya, mkoa na ujenzi wa shule za kisasa za ghorofa.

Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Khadija Ali Salum, alisema wanachama wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja wana kila sababu ya kumuunga mkono Rais Dk. Mwinyi na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza miradi mingi ya maendeleo mkoani humo.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid, alieleza kuwa serikali imeelekeza miradi mingi ya maendeleo Mkoa wa Kusini Unguja na tayari serikali imeahidi kujenga tangi kubwa la maji mkoani humo ambalo litamaliza changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo.

# Kusitishwa mradi wa ufugaji vipepeo waathiri vijiji 2

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** MUHEZA

WAFUGAJI wa vipepeo kutoka Kijiji cha Kwezitu na Msasa IBC Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, wamesema kusitishwa kwa mradi wa ufugaji wa vipepeo kumewaathiri kiuchumi.

Wamesema mradi huo ni mkombozi katika kukuza kipato na shughuli zingine za maendeleo vijijini humo.

Wakizungumza na waandishi wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JETI), waliotembelea Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Amani wilayani humo, chini ya ufadhili wa USAID Tuhifadhi Maliasili, walisema mradi huo unawasaidia kupata kipato na kusomesha watoto wao shule.

Jestina Gakara Ndeisaba, ni miongoni mwa wafugaji wa vipepeo wa Kijiji cha Kwezitu, alisema mradi huo umewatoa katika umaskini lakini hali sasa imekuwa ngumu baada ya mradi huo kusitishwa.

Alisema mradi huo ni mzuri na walikuwa na uhakika wa kupata kipato cha Sh. 300,000 kwa mwezi na kuwa na uhakika wa kuwaendeleza watoto wao kielimu pamoja na mahitaji mingine muhimu.

Mwanakijiji huyo alisema wakati wanafanya biashara hiyo, walikuwa wakiaminika kwa wafanyabiashara na walikuwa na uwezo wa kukopa vyakula dukani na kuaminiwa kwa sababu walikuwa na uhakika wa kupata fedha katika kipindi kifupi.

"Ulikuwa ni mradi mzuri sana mfano kama sasa sio msimu wa mavuno wa vyakula lakini tungekuwa na mradi wa vipepeo tungekuwa hatuna wasiwasi wa kupata fedha ya kujikimu kimaisha lakini sasa maisha ni magumu mno," alisema.

Aloyce Kibiriti Mwenyekiti wa Kijiji cha Msasa IBC, alisema mradi wa vipepeo ni rafiki mzuri wa mazingira na uliwafanya wananchi kutougusa msitu kwa shughuli za kijamii kwasababu ya kupata fedha zinazotokana na biashara ya vipepeo.

"Mradi wa vipepeo umewezesha kuwa na ofisi hii mnayoiona ambayo ni ofisi ya Ofisa Mtendaji wa kijiji hiki, hii inatokana na ile asilimia saba inayopatikana katika mradi huo katika huduma za maendeleo vijijini," alisema mwenyekiti huyo ambaye alikuwa mfugaji wa vipepeo.

Aidha, alieleza mradi huo umesaidia maendeleo ya kijiji hasa kwa vijiji saba vilivyozunguka ushoroba wa Delema ambao umesaidia pia kipato cha mtu.

Alisema kusitishwa kwa mradi huo umeleta masikitiko kwa wananchi wa vijiji vilivyozungukwa na ushoroba wa Delema kwa sababu kuna wanakijiji wamefanikiwa kujenga nyumba na kununua pikipiki za biashara.

Meneja Mradi wa Ufugaji wa Vipepeo, Amiri Said Sheghembe, alisema mradi huo ulikuwa chini ya kikundi cha kuhifadhi misitu na ni mradi wa kiuchumi na kijamii uliozishwa mwaka 2004 na malengo makuu ni kuikwamua jamii kiuchumi inayoishi kando ya misitu ya hifadhi.

Alisema mradi huo ni wa kwanza kwa Tanzania na asilimia 50 ya wanufaika ni wanawake na soko kubwa la vipepeo ni Bara la Ulaya na Amerika ambapo asilimia 65 ya mradi huo ukirudi kwa wafugaji wa vipepeo, asilimia 28 ni ya mradi ili ujiendeshe na asilimia saba kwa maendeleo ya jamii na vijiji husika huamua wenyewe itumike katika mradi gani.

Akitaja miongoni mwa mafanikio yaliopatikana kupitia mradi huo, alisema baadhi ya vijiji kama Kisiwani walitengeneza mradi mkubwa wa maji safi ya bomba, Kijiji cha Kwezitu na Msasa IBC walitumia kwa ujenzi wa madarasa ya shule na vijiji vingine walitumia kwa kutengeneza madaraja ambayo yanaunganisha wananchi kutoka kitongoji kimoja na kingine.

Alisema mradi huo pia ulieneza elimu ya ufugaji huo hadi visiwani Zanzibar kwa ajili ya kulinda Msitu wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani lakini pia ni kivutio kizuri kwa watalii visiwani humo.

Alisema ufugaji huo unaendana na uhifadhi wa misitu ambapo Msitu wa Amani kuna misitu mikubwa ambayo ni chanzo cha maji na jamii ya Mkoa wa Tanga wanatumia maji yanayotoka katika msitu huo.

"Jamii inayozunguka misitu kama hawatopata shughuli mbadala za kipato zitakazosaidia katika uhifadhi wataendelea kila siku kufanya uharibifu wa mazingira, ufugaji wa vipepeo unategemea uwepo wa misitu," alisema.

Aidha, alisema mradi huo ulikuwa na mauzo mazuri ambapo mauzo ya chini mwaka 2004 yalikuwa Sh.milioni 20, lakini kadri miaka inavyoenda mradi ulifikia thamani ya Sh.milioni 120 kwa mwaka hadi ulipositishwa na serikali mwaka 2006.



Mkurugenzi Mtendaji wa NCBA, Claver Serumaga (kulia), akimkabidhi zawadi ya heshima Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Dk. Saada Mkuya (kushoto), katika hafla ya wateja iliyoandaliwa na Benki ya NCBA kutangaza azma yao ya kuendelea kuwekeza katika sekta ya utalii Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana walioshindwa kufika chuo kikuu watengewa bajeti

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar, imesema itaendelea kutenga bajeti ya mikopo kuwasaidia vijana wanaokosa fursa ya kujiunga na elimu ya juu ili wafanikishe ndoto zao kwa ustawi wa maendeleo yao.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa, viwanja vya Maisara Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema serikali imejipanga kufanikisha lengo lake hilo licha ya ongezeko la kila mwaka la vijana wanaopata sifa za kujiunga na elimu ya juu.

Alisema, serikali imechukua jitihada mbali mbali kuimarisha ustawi wa vijana kwa kuwashirikisha kwenye sekta zote za maendeleo ikiwamo afya, elimu, kilimo, uvuvi, TEHAMA, ujasiriamali na michezo kwa kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa. Aidha, Dk. Mwinyi alieleza Serikali za SMZ na SMT zimeweka utaratibu maalum wa ajira, chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya Mwaka 2008 ambayo imetoa asilimia 21 ya ajira kwa vijana wa Zanzibar kwenye sekta za muungano.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya mwelekeo wa kiuchumi ya mwaka 2022 kupitia miradi ya fedha za ahueni za UVIKO- 19, vijana 13,870 walifanikiwa kupata ajira za muda kupitia miradi iliyowekezwa na serikali kupitia sekta mbalimbali za maendeleo.

Hata hivyo, Rais Dk. Mwinyi aliahidi kuanzishwa kwa sera mpya ya maendeleo ya vijana itakayozingatia mahitaji ya wakati wa sasa na ujao.

Pia alitoa wito kwa taasisi zote za umma na binafsi, washirika wa maendeleo, mabaraza ya vijana na asasi za maendeleo ya vijana, kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa sera hiyo kwa vitendo ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, aliahidi serikali kuendeleza fursa kwa vijana, kuwasimamia, kuratibu na kupunguza changamoto zinazowakabili.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Vijana, Yunus Juma Ali aliwataka vijana kuendeleza heshima kwenye jamii, kuvumiliana na kuyasema mambo yenye uhakika kwa kufanyia utafiti na kujiridhisha kabla ya kuzungumza.

# Serikali kuchukua hatua kwa watakaojaribu kuiba mitihani

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeahidi kuchukua hatua kali zaidi kwa mtu yeyote atakayejaribu kuiba mitihani ya darasa la saba inayotarajiwa kufanyika katikati ya mwezi ujao.

Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Abdul Maulid, alitoa onyo hilo wakati wa mahafali ya 19 ya Shule ya Msingi Tusiime ya Tabata, mwishoni mwa wiki.

Alisema mtu yeyote atakayefanya udanganyifu kwenye mitihani hiyo au kuiba hataachwa salama, hatua kadhaa zimeshachukuliwa kama mfano kwa waliojaribu kufanya udanganyifu kama huo.

"Awe mwanafunzi, awe mzazi, mwenye shule au mwalimu sisi hatutamwacha salama kwa hiyo watu wafuate utaratibu waache ujanja ujanja wawaandae wanafunzi wafanye mitihani yao wenyewe," alisema Maulid.

Alimsifu Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Albert Katagira kwa uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye elimu, hali aliyosema inaisaidia serikali kwenye maendeleo ya sekta ya elimu.

Alisema matokeo mazuri ya kitaaluma ya shule hiyo yamekuwa kivutio kikubwa kwa wazazi wengi kupeleka watoto wao, lakini aliwataka kulipa ada kwa wakati ili kumwezesha mwekezaji huyo kulipa walimu.

Vile vile, aliwataka wazazi kuchangia chakula shuleni ili kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa utulivu na hatimaye kupata matokeo mazuri kwenye mitihani yao ya kitaifa.

Alhaji Maulid aliipongeza Shule ya Tusiime kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula kwa wakati hali ambayo inasaidia maendeleo mazuri kitaaluma na kufanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani ya ndani ya shule na ya kitaifa.

Alizitaka shule zote nchini kuajiri maofisa ushauri nasaha ili kuwapa ushauri wanafunzi wanaofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia majumbani.

"Nawapongeza hapa Tusiime mnaye ofisa ushauri nasaha mmemwajiri na wengine kote nchini waige mfano huu kwasababu watoto wanaotendewa vitendo vya ukatili ni wengi ingawa matukio hayo huwa hayaripotiwi," alisema Maulid.

Alisema ameshangazwa na wanafunzi wa shule hiyo ya msingi wanavyomudu kuzungumza Kiingereza kama wako kwenye vyuo vikuu.

Aliwakumbusha wazazi kuwa karibu na kuzungumza na watoto wao kuhusu madhira wanayopata wakiwa nyumbani kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa wazazi wengi hawana muda wa kukaa na watoto.

Alisema kuna matukio mengi ya watoto kufanyiwa ukatili wa kijinsia tena na ndugu wa karibu na familia husika, lakini kwa kuwa wazazi hawana muda wa kukaa na watoto wao wakazungumza matukio hayo yanaendelea kutokea watoto hawasemi.




Mratibu na Mkuu wa Kanda ya Dar es Salaam wa Kampuni ya Ulinzi, Usalama na Uokoaji ya Nguvu Moja, Camil Alphonce (katikati) akiwa na maofisa ulinzi wa kampuni hiyo, Irine Henry (kushoto) na Eugine Alex, wakifurahia tuzo ya ushindi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nguvu Moja yatwaa tuzo ubora kimataifa barani Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya huduma za ulinzi na usalama ya Nguvu Moja jijini Dar es Salaam imetwaa tuzo ya ubora wa huduma za ulinzi, usalama na uokoaji kwa kampuni za kiwango cha kati katika utafiti wa kupata kampuni bora 100 za huduma ya ulinzi, usalama na uokoaj barani Afrika.

Utafiti huo uliofanywa na Kampuni ya Eastern Star Consulting Group Limited (ESCGL) ya jijini Dar es Salaam na kujumuisha zingine za ulinzi, usalama na uokoaji barani Afrika, umeonyesha Nguvu Moja kuongoza katika ubora wa huduma kwa kujali maslahi ya wateja kwa mujibu wa mikataba yao.

"Rekodi zinaonyesha katika kampuni za ulinzi ngazi ya kati kampuni ya Nguvu Moja imewekeza vyema katika vitendea kazi, mafunzo na motisha kwa wafanyakazi wake. Hii imeifanya kampuni kuweza kutoa huduma kwa mujibu wa mikataba yake na wateja na kuwa na ubora wa hali ya juu," alisema Deogratius Killawe, Mkurugenzi Mtendaji wa African Company of the Year Award.

Meneja Uratibu wa Kampuni hiyo, Camil Joseph, ambaye ni Mkuu wa Kanda ya Dar es Salaam, alisema kampuni yake ina zaidi ya miaka 10 katika utoaji wa huduma za ulinzi na usalama hasa katika uchimbaji madini Kanda ya Ziwa, inastahili tuzo hiyo kwa kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa.

"...Tumekuwa tunatoa huduma za ulinzi, usalama na uokoaji kwa ufanisi mkubwa kwa kampuni za madini kama Tanzanite One huko Mirerani, Barrick Gold Mine Limited yenye ubia na Serikali ya Tanzania," alisema.

Kampuni ya Nguvu Moja Security Services licha ya kuhudumia migodi pia huduma zake zinagusa nyumba za ibada na sasa inatoa huduma za ulinzi, usalama na uokoaji kwa Kanisa Katoliki St. Peters Oysterbay na Ubalozi wa Vatican jijini Dar es salaam.

Uongozi wa kampuni ya Nguvu Moja umetoa shukrani kwa Mkurugenzi Mtendaji na timu yake katika 'African Company of the Year Award' kwa mwaka 2022/23 kwa kufanya utafiti ulioiibua kampuni hiyo na kuihamasisha kulenga kufanya vyema zaidi katika utendaji wa majukumu yake kwa wateja kwa miaka ijayo.

# LATRA yatoa kifungoni mabasi 9 ruti za usiku

**Na Pilly Kigome**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhrini (LATRA) imerudisha ratiba za ruti za saa tisa usiku kwa mabasi tisa ya kampuni ya Ally's Star na Katarama Luxury.

Juni 19, mwaka huu LATRA walifungia mabasi ya kampuni hizo ratiba zinazoanza safari zake majira hayo kutokana na ukiukwaji wa sheria.

Ilidaiwa kutokana na kifungu cha 5(1)(b) na 6(b) cha sheria, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, sura ya 413 LATRA ina mamlaka na jukumu la kuuhisha na kufuta vibali na leseni za usafirishaji kwa kukuza usalama wa sekta zinazodhibitiwa kwa watumiaji wa huduma.

Akiongea na vyombo vya habari, Kaimu Mkuu wa kitengo cha Uhusiano, Salum Pazi, alisema wamekuwa wakifuatilia utoaji wa huduma wa mabasi hayo kwa ukaribu ikiwa na uzingatiaji ratiba zao za kuanza safari, utumiaji wa taarifa katika mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari, mwendokasi wa magari na matumizi ya kutufe cha uchambuzi wa dereva (I-Button).

LATRA pia imetoa onyo kali kwa kampuni saba za mabasi ya abiria kutokana na ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu ikiwamo na mwendokasi uliopitiliza wakiwa safarini. Kampuni hizo ni New Force, Capricorn, Frosterley, Abood, Baraka Classic, Nyahunge Express na Kilimanjaro.

LATRA iligongea msumari zaidi kwa kuwapa onyo ya mwisho kwa kampuni ya New force kutokana na historia ya kupata matukio mengi ya ajali.

"Agosti 7, mwaka huu moja ya basi lake lilisababisha ajali kutokana na uzembe wa dereva, vitendo hivyo havivumiliki," alisema Pazzy.

Alisema LATRA inataka kampuni zote za mabasi ya abiria kufuata sheria na taratibu ili waweze kutoa huduma bora na kuhakikisha usalama wa abiria na mali zao.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni Ally's Star, alishukuru kwa kurejesha ratiba hizo na kuahidi kujirekebisha kutokana na makosa ga awali.

Meneja wa kampuni Katarama Luxury, Elimboto Mtatuu, alikiri kulikuwa na udhaifu katika uendeshaji wa kampuni hizo.

"Tunaishukuru LATRA kwa kurudishiwa ruti hizo kwani tumejifunza kutokana na makosa," alisema.

HABARI KITAIFA/ KIMATAIFA

## Utawala wa kijeshi Niger watishia kumuua Bazoum

**NIAMEY,** Niger

UTAWALA wa kijeshi umetishia kumuua Rais aliyeondolewa madarakani, Mohamed Bazoum, endapo Jumuiya ya Ukanda wa Afrika Magharibi (ECOWAS) utaiingilia Niger kijeshi.

Inaelezwa kuwa mvutano unazidi kuongezeka kati ya utawala mpya wa kijeshi wa Niger na ECOWAS ambayo imeamuru kutumwa kwa wanajeshi kurejesha demokrasia nchini humo.

Jumuiya ya ECOWAS ilisema kuwa imeamua kupeleka kikosi cha kukaa tayari kinacholenga kurejesha utaratibu wa kikatiba nchini Niger, baada ya muda wa masharti yake ya kumrejesha madarakani kumalizika siku chache zilizopita.

Maofisa wawili wa nchi za Magharibi waliiambia shirika la habari la Associated Press kwamba utawala wa Niger ulimwambia mwanadiplomasia mkuu wa Marekani kwamba wangemuua Bazoum ikiwa nchi jirani zitajaribu kuingilia kati kijeshi kurejesha utawala wake. Haijulikani ni lini au wapi kikosi cha ECOWAS kingetumwa, na jinsi ripoti za vitisho dhidi ya Bazoum zingeathiri uamuzi wa jumuiya hiyo yenye wanachama 15 kuingilia kati.

Wataalamu wa mizozo wanasema kikosi hicho kinaweza kuwa na wanajeshi 5,000 wakiongozwa na Nigeria na kinaweza kuwa tayari ndani ya wiki chache.

Baada ya mkutano wa ECOWAS, Rais wa nchi jirani ya Ivory Coast, Alassane Ouattara, alisema nchi yake itashiriki katika operesheni hiyo ya kijeshi pamoja na Nigeria na Benin.
**VOA**



Moto ulivyoteketeza kisiwa cha Maui, Hawaii nchini Marekani huku miti ikionekana kuathiriwa zaidi. Idadi ya waliofariki katika moto huo yafikia watu 80. **PICHA: MTANDAO**

WANANCHI KUPISHA HIFADHI

# Fidia bil. 26/- yaibua shangwe Mbarali

**Na Halfani Chusi**

BAADA ya kuwapo mvutano wa muda mrefu kati ya askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na wakazi wa Wilaya ya Mbarali, hususan wanaopakana na Mbuga ya Ruaha, serikali imeamua kuwalipa fidia, waondoke.

Uamuzi huo uliotangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan Agosti 8, mwaka huu wakati wa kufunga maonesho ya kimataifa ya wakulima, wafugaji na wavuvi, maarufu Nanenane jijini Mbeya, umepokewa kwa mikono miwili na wakazi wa Mbarali wanaopaswa kupisha shughuli za uhifadhi kutokana na vijiji vyao kuingilia mipaka ya Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Katika hotuba yake siku hiyo, Rais Samia aliahidi serikali itatoa Sh. bilioni 26 kwa ajili ya fidia kwa wanakijiji hao ili kupisha eneo la hifadhi.

"Nimepokea maombi kadhaa ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. La kwanza, alikuwa anaomba fidia kule Mbarali na mshauri wangu wa siasa na mambo ya jamii kwa sababu aliwahi kuwa Waziri wa Ardhi, akaniletea tathmini ya fidia inayotakiwa pale.

"Nikateta na Waziri wa Ardhi wa sasa (Dk. Angelina Mabula). Idadi ni hiyohiyo, Sh. bilioni 26. Sasa mkuu wa mkoa, mimi ninakwenda kutafuta hizi bilioni na pengine mapema mwezi ujao (Septemba 2023) tunaweza tukaanza kulipa hizi fidia.

"Kwahiyo, Waziri wa Ardhi (Dk. Mabula) na timu yako mjipange ili tuweze kwenda kufanya hiyo kazi pale. Kwahiyo, fidia Mbarali zinakwenda kulipwa. Nitakwenda kuingia kwenye vikapu nichange huko mpaka zipatikane," Rais Samia aliahidi.

Ni hatua zilizochukuliwa na serikali ikiwa ni miezi miwili tangu Nipashe ilipochapisha ripoti kuhusu madhila wanayotendwa wakazi wa Kijiji cha Mwanavala, wilayani Mbarali na askari wa TANAPA, yakijumuisha kuchukuliwa mifugo yao na kuteswa kwa vipigo na kuunguzwa kwa mapanga ambayo askari hao walidaiwa kuyapasha katika injini ya chopa.

Ni ukatili uliomlazimu aliyekuwa Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega (marehemu) kutaka kauli ya serikali bungeni Mei 11 mwaka huu dhidi ya madai yake kuhusu wananchi wanaoteswa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliunda timu ikiongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, kuchunguza na kurejesha taarifa kwa hatua zaidi, huku watetezi wa haki za binadamu wakishinikiza serikali kuchukua hatua kutatua mgogoro huo wa muda mrefu.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera, alisema, "... zitakapotolewa fedha hizo ndipo tutajua ni kata ngapi zinapaswa kuhamishwa. Kwa kuwa sasa (suala hili) linafanyiwa kazi, ngoja tusubiri jambo likamilike, tutakapoanza huo mchakato tutatoa taarifa.

"Tutawatangazia watu watajua ni maeneo gani wanapewa fidia na wapi wanahamishiwa. Kila kitu kitakuwa hadharani, lakini kwa sasa tuliache, tusubiri mwezi ujao ambao serikali imeahidi. Baada ya hapo tutakuja na taarifa rasmi."

**MWITIKIO KIJIJINI**

Muda mfupi baada ya Rais Samia kutoa ahadi ya kulipa fidia kwa wananchi wa Mbarali watakaohamishwa hifadhini, mwandishi wa habari hizi alizungumza na wakazi wa Kijiji cha Mwanavala, akiwamo Lekake Luopashe aliyesema uamuzi huo wa serikali ni mzuri na unaleta amani kwao.

"Tumefurahi baada ya kumsikia Rais kwenye Maonesho ya Nanenane akitangaza kwamba Septemba tutalipwa. Amani imetawala. Tunasubiri muda ufike tuambiwe wapi pa kwenda tukaanze makazi mapya.

"Inatia faraja sana kwa serikali inapokuwa na usikivu wa namna hii. Watu walikuwa wanashindwa kuhama kwa sababu hawajalipwa na hawajajua wapi pa kuelekea," alisema Loupashe.

Naye Anna Seba - mkazi wa kijiji hicho, aliomba serikali kukamilisha huduma za kijamii na mazingira mazuri kwa ajili ya malisho ya mifugo yao huko watakakohamishiwa.

"Tumesikia, ni uamuzi mzuri, tena kaongea Rais mwenyewe. Ina maana hapo sasa mchakato umeiva kuliko wangeamua kututimua bila kutuambia wapi pa kwenda bila kutulipa fidia zetu. Tunasubiri utekelezaji ili tuhamie huko tuendelee na maisha yetu," alisema.

**KAULI YA LHRC**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimekuwa kikifuatilia mvutano huo kati ya wananchi na askari wa TANAPA, hata kuwa miongoni mwa watetezi wa haki za binadamu waliotoa kauli ya kuitaka serikali ichukue hatua Mei mwaka huu.

Hatua ya kuwalipa fidia wananchi iliyochukuliwa na serikali, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, anapongeza ni uamuzi mzuri katika kutatua migogoro kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi nchini.

"Nimepokea vizuri na kwa mtazamo chanya umuzi wa serikali kwa sababu yaliwahi kutokea mateso na mauaji kule (Mbarali). Watu walipigwa na kuteswa kutokana na mgogoro wa ardhi kati ya askari wa wanyamapori na wanakijiji.

"Lakini kuelekea kwenye hatua hiyo ya kutoa fidia, ninashauri kuwe na vikao vya awali, wawashirikishe wananchi hatua kwa hatua, vifanyike vikao vya mara kwa mara ngazi ya kijiji na kata.

"Kuwe na mashauriano ili baadaye yasije yakatokea tena kama masuala ya Ngorongoro na Loliondo. Watu waambiwe watahamishiwa wapi na watalipwa shilingi ngapi, wakae wanajua na kwa kuridhia, wasiwalazimishe tu," Dk. Anna alitoa angalizo katika mazungumzo na mwandishi mwishoni mwa wiki.

Alisema utaratibu huo wa vikao na wanakijiji utasaidia kuepusha kuibuka tena migogoro... "mara huyu hataki kuhama, huyu amegoma kupokea malipo kwa sababu kaona hayamtoshi".

Mkurugenzi huyo pia aliunga mkono hoja ya mwanakijiji wa Mwanavala, Anna Seba, kwamba wanakohamishiwa wananchi hao kuwe rafiki kwao kuishi - makazi yawe na huduma za kijamii zinazojumuisha maji, umeme, shule, kituo cha afya na kuzingatia uendelevu wa mifugo yao na shughuli zao za kilimo.

# NAMUNGO YAPANIA KUREJEA MICHUANO YA CAF MWAKANI

**Na Saada Akida, TANGA**

MABOSI wa Namungo FC wamesema kikosi chao kipo tayari kuanza msimu mpya mwaka 2023/24 baada ya kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kuwania taji hilo linalosakwa na klabu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Namungo FC inayoongozwa na kocha msaidizi wa zamani wa Yanga, Cedric Kaze, itafungua pazia la Ligi Kuu Bara kesho kwa kuvaana na Maafande wa JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko, Ruangwa mkoani Lindi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Denis Kitambi, alisema wamekuwa na maandalizi mazuri ambayo yamewasaidia kutengeneza muunganiko mzuri wa nyota wa zamani na wapya.

Kitambi alisema kwa kushirikiana na bosi mpya (Kaze), wameendelea kujiimarisha na wanaamini wako imara kwa ajili ya kupambana kusaka matokeo chanya katika kila mechi watakayocheza.

Alisema malengo yao ni kuona timu inafanya vyema kwa kukata tiketi ya kushiriki kwenye mashindano ya kimataifa mwakani.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tumecheza michezo ya kirafiki ambayo imetupa mwanga wa kuona ubora wetu na kuongeza pale penye madhaifu ili tuwe imara, kila kitu muhimu kimefanyika kuelekea mchezo wetu dhidi ya JKT Tanzania," alisema Kitambi.

Aliongeza wanafahamu ligi itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu imejiandaa vizuri na kufanya usajili wa kuboresha vikosi vyao.

Alisema wanawaheshimu JKT Tanzania kwa sababu wana uzoefu na hii inatokana na wao kuwahi kucheza Ligi Kuu Bara misimu ya nyuma.

"Hatutaichukulia kama timu ndogo kwa sababu walikuwapo muda mrefu kwenye ligi, walishuka na kupanda tena, imefanya usajili mzuri na wana benchi la ufundi imara, tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunabakiza alama tatu nyumbani," alisema kocha huyo.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazochezwa kesho ni kati ya Ihefu dhidi ya Geita Gold wakati Dodoma Jiji itawakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa Jamhuri.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Tusiime iliyoko Tabata wakitumbuiza katika mahafali ya 19 ya wenzao wanaomaliza darasa la saba mwaka huu yaliyofanyika mwishoni mwa wiki, Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tusiime yapongezwa kuibua vipaji

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeipongeza Shule ya Tusiime ya Tabata, Dar es Salaam kwa kuibua vipaji na kuzitaka shule nyingine nchini kutenga muda wa michezo kwa wanafunzi ili iwe rahisi kubaini na kuibua vipaji vipya, imeelezwa.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Abdul Maulid, katika mahafali ya 19 ya Shule ya Msingi Tusiime jijini.

Maulid alisema amefurahishwa na vipaji mbalimbali alivyoona katika shule hiyo na kuagiza shule nyingine kuiga mfano huo kwa kutenga muda wa wanafunzi kushiriki michezo na sanaa.

"Nawaagiza wamiliki wa shule za msingi na sekondari waige mfano wa shule za Tusiime kwa kuweka kipaumbele katika kuibua vipaji mbalimbali vya wanafunzi kwenye michezo na muziki," alisema.

Aliongeza wanafunzi wenye vipaji mbalimbali wameonekana kupitia mahafali hayo na endapo vitaendelezwa wanaweza kupatikana wasanii wakubwa nchini.

"Siku za kusoma kwa mtoto zinajulikana kwa hiyo muda mwingine mtoto aachwe acheze na watengewe muda wa kucheza na viongozi watambue kucheza ni sehemu ya masomo siyo kupoteza muda," aliongeza ofisa huyo.

Mwanafunzi mmoja wa darasa la saba alionyesha kipaji chake kwa kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali ya yanayohusu michezo nchini na Ligi Kuu England.

## Mbeya City FC yalia kuporwa wachezaji

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Mbeya City umezionya baadhi ya timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kusajili wachezaji wao bila kufuata taratibu zilizowekwa na mamlaka za mpira wa miguu.

Klabu hiyo ambayo imeshuka daraja imesema haina tatizo na wachezaji wake wanaotaka kuondoka na wanasisitiza taratibu zilizowekwa zifuatwe kabla ya wao hawajawachukulia hatua za kisheria.

Mwenyekiti wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, alisema kuna klabu zimekiuka kanuni kwa makusudi kwa kuwasajili wachezaji wao waliokuwa na mikataba halali.

"Klabu ya Mbeya City inapenda kuwajulisha wadau wote wa michezo wa mpira wa miguu kumeibuka mtindo wa baadhi ya timu kusajili wachezaji wetu wenye mikataba bila maridhiano na klabu husika kama takwa la kanuni ya 2021 inavyohitaji.

Ikumbukwe kuwa wachezaji walisaini mikataba yao na klabu yetu bila kujali timu inacheza ligi daraja gani," alisema Kimbe katika taarifa yake rasmi iliyotolewa jana.

## ACT yakumbushia maslahi wanawake

**Emmaloveness Gaston na Mwanahamisi Mussa**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, ameomba kuboreshwa kwa maslahi ya wachezaji wanawake ili kuongeza ushiriki wao katika michezo mbalimbali ni mdogo ukilinganisha na wanaume ikiwamo mpira wa miguu.

Akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Semu alisema bado inahitajika hamasa ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika michezo kwa kuwapa maslahi yanayoendana na wanaume.

"Bado hatuna utaratibu endelevu wa kuwatambua na kuwaendeleza wanasoka wanawake, kuna mwitikio mdogo na maslahi duni kwa wachezaji wanawake tofauti na wenzao wanaume, hili tunatakiwa kuliangalia zaidi," alisema Semu.

Aliongeza kwa kuitaka serikali kuanzisha shule za michezo angalau moja kwa kila kanda ili kuwezesha vijana kupata mafunzo sahihi kuanzia ngazi ya awali pamoja na kuboresha miundombinu.

"Upungufu wa viwanja vyeye ubora na hadhi ya kimataifa unashusha thamani ya mchezo wa mpira wa miguu pamoja na kupoteza fursa mbalimbali za kuandaa mashindano ya kimataifa, " alisema kiongozi huyo ambaye alijitambulisha kama shabiki wa Simba.

## ZISIKUPITE

### CAICEDO NJIA MOJA
CHELSEA iko mbioni kumsajili kiungo wa kati wa Brighton, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21 kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 115 huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ecuador akijiandaa kuitosa Liverpool. **(Sunday Telegraph)**

### CAICEDO KUZEEKEA CHELSEA
MAKUBALIANO kati ya Moises Caicedo na Chelsea ni ya mkataba hadi Juni 2031 pamoja na chaguo la mwaka wa ziada na maslahi binafsi yalikubaliwa Mei. **(Fabrizio Romano)**

### LIVERPOOL, CHELSEA VITANI
LIVERPOOL inatarajiwa kushindwa na Chelsea katika harakati za kumnunua kiungo wa kati wa Ubelgiji, Romeo Lavia, mwenye umri wa miaka 19, ambaye anatazamiwa kuondoka Southampton kwenda Stamford Bridge kwa ada ya pauni milioni 55. **(Mail)**

### SCHMEICHEL KUMRITHI KEPA
GOLIKIPA wa Denmark, Kasper Schmeichel, mwenye umri wa miaka 36 anatazamiwa kujiunga na Chelsea kutoka Nice kuchukua nafasi ya Kepa Arrizabalaga (28), ambaye atajiunga na Real Madrid kwa mkopo wa msimu mzima. **(Guardian)**

### ADAMS ATAKIWA BRIGHTON
KLABU ya Brighton inavutiwa na Tyler Adams mwenye umri wa miaka 24 kutoka Leeds United baada ya Chelsea kuachana na mpango wao wa kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani, pamoja na nyota wa Ajax na Ghana, Mohammed Kudus (23). **(Independent)**

### CITY YAMFUATA PAQUETA
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameweka usajili wa kiungo wa kati wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta, mwenye umri wa miaka 25 kuwa kipaumbele chake cha juu baada ya Kevin de Bruyne kuumia katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Burnley. **(Mchezo)**

### WAHI ANUKIA WEST HAM
KLABU ya West Ham iko tayari kuwasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Montpellier, Elye Wahi, mwenye umri wa miaka 20, ambaye analengwa na Chelsea na Eintracht Frankfurt. **(L'Equipe)**

### KANE KUITAJIRISHA BAYERN
BAYERN Munich ina imani itapata fedha nyingi kutokana na mauzo ya jezi zenye jina la Harry Kane, na kuwasaidia kurejesha ada kubwa ya uhamisho waliyolipa Tottenham Hotspur kwa nahodha huyo wa England mwenye umri wa miaka 30. **(Sunday Mirror)**

### SPURS YASAKA STRAIKA
KLABU ya Tottenham Hotspur itavunja rekodi yao ya ada ya uhamisho ya pauni milioni 55 ili kumsajili mshambuliaji wa kiwango cha juu kuchukua nafasi ya Harry Kane baada ya straika huyo kuuzwa Bayern Munich. **(Football Insider)**

### EVERTON YAMTAKA IWOBI
KLABU ya Everton bado inaendelea na mazungumzo na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Alex Iwobi, mwenye umri wa miaka 27 kuhusu mkataba mpya huku akiingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake wa sasa. **(Liverpool Echo)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ATOA SABABU KUMBAKISHA TIMBER

Kocha huyo asema uamuzi wake ulitokana na ruhusa ya madaktari na...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta ametetea uamuzi wake wa kutomtoa, Jurrien Timber mapema katika ushindi wa mabao 2-1 ambao Arsenal ilipata dhidi ya Nottingham Forest baada ya Mholanzi huyo kupata jeraha la goti, Jumamosi.

Pambano lake na Brennan Johnson katika kipindi cha kwanza lilimfanya Timber achechemee, lakini aliendelea hadi dakika ya 50 kabla ya kutolewa nje, huku mchezaji wa kimataifa wa Japan, Takehiro Tomiyasu, akichukua nafasi yake.

Baada ya mchezo huo, Arteta aliulizwa kama alipaswa kumtoa Timber mapema, lakini akasisitiza beki huyo aliruhusiwa kuendelea na madaktari.

"Madaktari walimtazama na walifurahi kwa yeye kuendelea," alisema bosi huyo wa Arsenal.

"Mara moja katika hatua ya kwanza ya kipindi cha pili alifanya harakati na ilikuwa ya kuchekesha. Tulimtoa nje moja kwa moja na sasa inabidi tumtathmini na kuona ana nini."

Tomiyasu aliingia akitokea benchi kuchukua nafasi ya Timber, huku Arteta akiamua kutomwita beki wa kati wa Brazil, Gabriel Magalhaes, ambaye kwa mshangao alianzia kwenye benchi.

Arteta alithibitisha Gabriel hakuwa majeruhi na aliachwa tu kama uamuzi wa busara.

"Ndio, tulitarajia mchezo ambao ulifanyika na tulihitaji mtu mwingine katika safu ya kati kufanya kile tulichofanya vyema zaidi," alisema.

Mchezaji mmoja wa kwanza ambaye alifurahia mechi bora ya kwanza ya ligi akiwa na rangi za Arsenal alikuwa kiungo, Declan Rice, ambaye alimvutia sana kocha wake.

"Umemwona leo (juzi), sijui ilikuwa baada ya dakika mbili au baada ya kumi, lakini jinsi anavyosonga, jinsi anavyocheza na kujumuika kwenye chumba cha kubadilishia nguo nadhani anafurahia nafasi hiyo," alieleza Arteta.

"Labda angefunga mabao mawili leo (juzi), na alikuwa na furaha kubwa sana kwa kile alichokuwa akikifanya uwanjani."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
WOLVERHAMPTON
1 | 1.36
X | 5.08
2 | 8.47

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HARRY KANE APOKELEWA NA KIPIGO BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

HARRY Kane alikosa taji la kwanza lililokuwa likisubiriwa kwa muda mrefu katika mchezo wake wa kwanza akiwa na Bayern Munich baada ya timu yake mpya kufungwa mabao 3-0 na RB Leipzig katika mechi ya kuwania Kombe la Super Cup la Ujerumani iliyochezwa juzi nchini humo

Nahodha huyo wa England amesaini mkataba wa miaka minne huku kukiwa na wasiwasi wa vyombo vya habari saa chache mapema na akatokea benchi kipindi cha pili, lakini hakuweza kuzuia kushindwa kwa mechi ya ufunguzi wa msimu dhidi ya washindi hao wa Kombe la Ujerumani.

Badala yake alikuwa, Dani Olmo wa RB Leipzig ambaye alifunga hat trick na kuipa Leipzig ushindi wa kwanza wa Super Cup.

Matokeo hayo yalimwacha Kocha wa Bayern, Thomas Tuchel, akiwa amefura kwa hasira, akisema inaonekana timu hiyo haikufanya lolote katika kipindi chao cha wiki nne cha maandalizi ya msimu mpya.

"Ni shida kubwa kwa sababu nahisi kama hatujafanya chochote katika wiki nne zilizopita," alisema Tuchel.

"Siwezi kuielezea. Haikutosha katika kila idara. Sijui ni kwa nini. Hakuna uhusiano kati ya hali yetu na mtazamo wetu kuelekea mchezo na uchezaji wetu uwanjani.

"Sio vizuri. Ni jambo baya zaidi kwa sababu kuna tofauti kubwa."




Huku Bayern wakipoteza nafasi, kocha Thomas Tuchel alimleta Kane, ambaye uhamisho wake uligharimu rekodi ya Bundesliga yaeuro milioni 100, na alipoingizwa dakika ya 64 alishangiliwa kwa nguvu na mashabiki wa Bayern.

Lakini hakuweza kufanya chochote na aligusa mpira mara tatu pekee, na ni Olmo ndiye aliyefunga tena, safari hii kwa mkwaju wa penalti dakika nne tu baadaye, na kuihakikishia timu yake taji la kwanza la msimu huu.

Bayern wataanza msimu wao wa Bundesliga dhidi ya Werder Bremen, mechi itakayochezwa Ijumaa.

# Ancelotti amsifu Bellingham

**BILBAO, Hispania**

CARLO Ancelotti alimsifu Jude Bellingham ana kiwango "bora" baada ya kiungo huyo wa kati wa England kufunga na kumfanya kuwa mchezaji bora kwenye mechi yake ya kwanza ya ushindani akiwa na Real Madrid katika ushindi wa mabao 2-0 ugenini dhidi ya Athletic Club hapo juzi.

Rodrygo aliifungia Madrid bao la kuongoza dakika ya 28 mjini Bilbao kabla ya Bellingham kuongeza bao la pili dakika nane baadaye.

Mabao hayo yaliipa Madrid pointi zote tatu katika mchezo wao wa ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, huku mlinzi Éder Militão akichechemea kwa kilio kipindi cha pili kutokana na jeraha la goti.

"Bellingham ni bora," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Ni mchezaji mzuri na mwenye haiba kubwa, ni mchezaji mwenye ubora. Ni usajili muhimu sana... Ana tabia dhabiti, anahisi kama amekuwa hapa kwa muda mrefu."

Madrid ililipa euro milioni 103 za awali, na uwezekano mwingine wa euro milioni 30 katika vigezo kumsajili Bellingham mwenye umri wa miaka 20 kutoka Borussia Dortmund msimu huu wa joto, akiwa nyongeza yao kwenye kikosi pamoja na Arda Güler, Joselu, Fran García na Brahim Díaz.

"Siku zote nimefundishwa kuwa ukijaribu kugonga shabaha basi unajipa nafasi," Bellingham aliiambia Real Madrid TV alipoulizwa kuhusu bao lake la kwanza.

"Sikuwa na mawasiliano mazuri, nilipata bahati kidogo, lakini nilifikia lengo."



Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# MGUNDA KUINOA SIMBA QUEENS, IKINASA WATATU

**Na Saada Akida, TANGA**

MKURUGENZI wa Ufundi wa Simba, Juma Mgunda, inaelezwa sasa amepewa jukumu jipya la kuiongoza Simba Queens, akichukua mikoba iliyoachwa na Mganda, Charles Lukula, imefahamika.

Mgunda alikuwa Kocha Msaidizi wa Wekundu wa Msimbazi, lakini mabosi wa klabu hiyo wameamua kumpa majukumu mapya.

"Ni kweli kwa sasa kikosi cha timu ya wanawake amekabidhiwa majukumu Mgunda, atakuwa akifundisha timu hiyo huku akiendelea na majukumu yake mengine ya ufundi kwa timu zote za Simba," kilisema chanzo chetu.

Simba Queens ilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Masala Princess katika Tamasha la Simba Day ikiwa chini ya Kocha Msaidizi, Sophia Mwasikili.

Hata hivyo Nipashe ilipomtafuta Meneja wa timu hiyo, Selemani Makanya, alisema bado hawajapewa taarifa rasmi kuhusu kocha anayechukua mikoba ya Lukula.

"Suala hili bado liko katika mikono ya viongozi, wameniambia tayari kocha ameshapatikana na ataanza majukumu yake baada ya kuanza kambi hivi karibuni," alisema meneja huyo.

Aliongeza wamefanya usajili mzuri kwa kuongeza nguvu katika kikosi chao kwa kuzingatia mapungufu waliyoyabaini katika msimu uliomalizika.

Aliwataja wachezaji wapya waliosajiliwa ni Isabelle Diakiese kutoka Bikira FC ya DRC, Ritticia Nabbosa wa Fountain Gate Princess na Joanitha Ainembabazi aliyekuwa Ceasiaa Queens.



Mchezaji wa Timu ya Sekondari ya Majani ya Chai, Frida Gabriel (kulia), akiwania mpira dhidi ya mpinzani wake kutoka Shule ya Buza, Leila Shomari, katika mashindano ya mchezo wa magongo kwa shule za sekondari yanayofanyika kwenye viwanja vya JMK Park, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mashujaa yazidi kuimarika

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mashujaa FC imelazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Inter Star kutoka Burundi katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, ikiwa ni kilele cha Tamasha la Mashujaa Day.

Ni siku ambayo mashabiki wa Kigoma, viongozi mbalimbali wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Thobias Andengenye, walipokusanyika kuifahamu timu yao kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pia timu hiyo ilifanya uzinduzi rasmi wa jezi watakazozitumia katika mechi za nyumbani na ugenini.

Mashujaa FC ilikuwa ya kwanza kupata bao dakika ya 29 kupitia kwa Idrissa Stambuli 'Banka' na wageni walisawazisha kipindi cha pili.

Kabla ya mechi hiyo kulikuwa na pambano la awali ambapo mabingwa wa soka wa mkoa kwa wanawake, Mwanga City Queens waliwafunga Mkongolo Queens mabao 2-0.

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 14/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 1869 | Dewa United vs Psis Semarang | 2.08 | 3.39 | 2.98 |
| 13:00 | 5286 | Bucheon vs Gyeongnam | 2.32 | 3.37 | 2.61 |
| 13:30 | 2558 | Cheonan City FC vs Gimpo Citizen | 3.54 | 3.08 | 1.99 |
| 15:00 | 1448 | Arema vs Rans Nusantara | 2.35 | 3.38 | 2.57 |
| 15:00 | 2561 | Crystal Palace U21 vs Manchester United U21 | 2.33 | 3.92 | 2.40 |
| 15:00 | 4597 | Lamphun Warrior vs Sukhothai FC | 1.79 | 3.43 | 3.83 |
| 16:00 | 2350 | Alashkert Martuni vs Van Yerevan | 1.52 | 3.93 | 5.31 |
| 16:00 | 3644 | Negeri Sembilan vs Selangor FC | 5.85 | 4.44 | 1.40 |
| 16:00 | 4198 | Birmingham U21 vs Watford U21 | 2.60 | 3.92 | 2.17 |
| 16:00 | 4632 | Kelantan FA vs Terengganu | 11.12 | 6.27 | 1.16 |
| 16:00 | 5084 | FC Samtredia vs Torpedo Kutaisi | 5.91 | 3.87 | 1.49 |
| 17:00 | 3667 | Shakhtar Donetsk vs Oleksandria | 1.31 | 4.65 | 7.48 |
| 18:00 | 2955 | Abha vs Al Hilal Riyadh | 5.21 | 4.27 | 1.55 |
| 18:00 | 5467 | Al Raed Club vs Al Ittihad Jeddah | 8.59 | 5.45 | 1.30 |
| 18:00 | 5492 | Ararat Armenia vs Pyunik Yerevan | 2.08 | 3.31 | 3.16 |
| 18:45 | 1735 | Cremonese vs Crotone | 1.46 | 4.37 | 6.25 |
| 19:00 | 1833 | Sampdoria vs Sudtirol | 1.82 | 3.44 | 4.28 |
| 19:00 | 2041 | VfB Lubeck vs Hoffenheim | 6.16 | 4.88 | 1.44 |
| 19:00 | 2374 | Novi Pazar vs FK Imt Novi Beograd | 1.76 | 3.08 | 4.64 |
| 19:00 | 5521 | Jahn Regensburg vs Magdeburg | 3.97 | 3.65 | 1.87 |
| 19:00 | 5994 | Homburg vs SV Darmstadt | 6.30 | 4.73 | 1.45 |
| 19:30 | 3044 | Nimes vs FC Martigues | 2.40 | 3.30 | 2.73 |
| 19:30 | 3849 | Nizhny Novgorod vs Akhmat Grozny | 2.53 | 3.07 | 2.71 |
| 20:00 | 1719 | Mjallby vs Malmo | 4.25 | 3.54 | 1.69 |
| 20:00 | 1741 | IFK Varnamo vs Degerfors | 1.76 | 3.58 | 3.83 |
| 20:00 | 1788 | Orebro SK vs Jonkopings Sodra | 1.90 | 3.56 | 3.82 |
| 20:00 | 3435 | Warta Poznan vs Ruch Chorzow | 1.88 | 3.28 | 3.68 |
| 20:00 | 4601 | Mirandes vs Alcorcon | 2.49 | 2.93 | 2.88 |
| 20:00 | 4874 | Viborg FF vs Hvidovre IF | 1.53 | 4.21 | 5.41 |
| 20:00 | 5573 | Orgryte IS vs Skovde Aik | 1.76 | 3.78 | 4.20 |
| 20:30 | 1365 | Dinamo Bucuresti vs Botosani | 2.44 | 3.02 | 2.87 |
| 20:30 | 3732 | Cadiz CF vs Alaves | 2.19 | 3.03 | 3.80 |
| 20:45 | 4389 | Moreirense vs Porto | 7.75 | 4.87 | 1.33 |
| 21:00 | 3126 | Deportivo Municipal vs Atletico Grau | 2.52 | 3.18 | 2.51 |
| 21:00 | 3460 | Jong PSV vs Telstar | 2.38 | 3.27 | 2.71 |
| 21:00 | 4170 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Utrecht | 1.58 | 4.00 | 4.72 |
| 21:00 | 4273 | Liverpool U21 vs Everton U21 | 1.33 | 5.40 | 5.60 |
| 21:00 | 4342 | Al-Ettifaq vs Al Nasr Riyadh | 3.23 | 3.49 | 2.11 |
| 21:00 | 5253 | Fatih Karagumruk vs Besiktas | 2.90 | 3.61 | 2.16 |
| 21:00 | 5583 | Alanyaspor vs Basaksehir | 2.69 | 3.42 | 2.37 |
| 21:00 | 5887 | Al Shabab Riyadh vs AL Akhdood | 1.53 | 4.30 | 5.45 |
| 21:15 | 4880 | Luka Koper vs NK Mura | 2.02 | 3.32 | 3.17 |
| 21:45 | 1326 | Osnabruck vs FC Koln | 3.85 | 3.91 | 1.84 |
| 21:45 | 5192 | Bordeaux vs Concarneau | 1.57 | 3.66 | 5.54 |
| 22:00 | 1458 | Manchester Utd vs Wolverhampton | 1.36 | 5.08 | 8.47 |
| 22:00 | 4452 | Spezia vs Venezia | 1.72 | 3.76 | 4.38 |
| 22:15 | 4905 | Torino vs Feralpisalo | 1.25 | 5.63 | 10.22 |
| 22:30 | 2824 | Tenerife vs Real Oviedo | 2.18 | 3.02 | 3.32 |
| 22:30 | 4308 | Atletico Madrid vs Granada | 1.37 | 4.91 | 8.50 |
| 22:45 | 1331 | Boavista vs Benfica | 9.35 | 5.37 | 1.26 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Agosti 14, 2023

Nipashe




**Arteta atoa sababu kumbakisha Timber**

UKURASA 21




# SALIM SHUJAA SIMBA IKIBEBA NGAO TANGA

●●●Adaka penalti tatu na kurejesha furaha Msimbazi baada ya...

**Na Faustine Feliciane, TANGA**

HUKU ikionekana inaanza msimu mpya bila ya mlinda mlango mzoefu, Ally Salim, amefanikiwa kuipa Simba taji la kwanza baada ya kudaka penalti tatu katika mechi ya fainali ya kuwania Ngao ya Jamii iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa jana usiku.

Simba imetwaa ngao hiyo kwa kuwafunga waliokuwa mabingwa watetezi, Yanga penalti 3-1 baada ya timu hizo kumaliza dakika 90 kwa sare ya bila kufungana.

" Sijui nisemeje, kwa namna nilivyo na furaha kuisaidia timu yangu kushinda mchezo huu wa Ngao ya Jamii, nawashukuru sana wachezaji wenzangu, makocha na mashabiki, hii kwangu ni historia" hiyo ni kauli ya Salim baada ya kuiongoza vyema timu yake hapo jana.

Salim aliibuka pia shujaa katika mchezo wa hatua ya nusu fainali kwa kudaka penalti moja walipokutana na Singida Fountain Gate FC.

Wachezaji wa Simba waliofunga penalti ni Mzamiru Yassin, Willy Onana na Jean Baleke huku aliyepata kwa upande wa Yanga ni Aziz Ki peke yake.

Upande wa Yanga waliokosa ni Khalid Aucho, Patrice Zouzou na beki wa pembeni Yaoyao huku kwa Simba ni Saido Ntibazonkiza na Moses Phiri.

Wakati huo huo, mabao yaliyofungwa na Prince Dube na Abdul Sopu yalitosha kuipa Azam FC ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Singida Fountain Gate FC katika mechi ya kusaka nafasi ya tatu ya mashindano ya kuwania Ngao ya Jamii iliyochezwa mapema kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani jana mchana.

Singida FG ambayo ilionyesha upinzani mkubwa katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya pili dhidi ya Simba ilikuwa ikipewa nafasi kupata matokeo chanya katika mechi ya jana, lakini hali ilikuwa tofauti.

Azam iliwachukua dakika moja tu kuandika bao la kwanza kupitia kwa Dube baada ya makosa ya safu ya ulinzi ya Singida Fountain Gate iliyojichanganya kutoa mpira ambao haukuwa na madhara yoyote kwao.

Kuingia kwa goli hilo la mapema kulifanya mchezo kuchangamka zaidi huku Singida Fountain Gate wakitaka kurudisha bao hilo na Azam wakipambana kuongeza goli lingine ili kuulinda ushindi wao.

Hata hivyo walikuwa Azam waliofanikisha mipango yao katika kipindi cha kwanza baada ya kufanikiwa kupata bao la pili kupitia kwa mwenyeji wa Tanga, Sopu.

## Safari ya ubingwa 2023/24 imewadia

**Na Faustine Feliciane, TANGA**

VITA ya kuwania ufalme wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu mpya wa mwaka 2023/2024 inatarajia kuanza rasmi kesho katika viwanja vitatu tofauti hapa nchini.

Mechi za ufunguzi wa ligi hiyo ni kati ya Ihefu SC dhidi ya Geita Gold FC wakati Namungo wakiwa nyumbani kwao kwenye Uwanja wa Majaliwa, Lindi wataikaribisha JKT Tanzania iliyorejea tena Ligi Kuu wakati Dodoma Jiji nao watawavaa 'Wagosi wa Kaya', Coastal Union.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kuanza msimu mpya na anafahamu utakuwa mgumu, wenye ushindani, lakini anaipa nafasi timu yake kufanya vizuri kutokana na aina ya kikosi walichonacho.

"Itakuwa ngumu, naweza kutabiri nani atakuwa bingwa mwanzo tu wa msimu, lakini natarajia ligi ngumu na yenye ushindani, nikizungumza kutokana na kikosi changu, tuna nafasi ya kufanya vizuri na kutetea ubingwa wetu," alisema Gamondi.

Gamondi alisema pamoja ya kuwa na kikosi kizuri, hii ni mara yake ya kwanza kufundisha katika Ligi ya Tanzania, amejipanga kukabiliana na changamoto zote ili kufikia malengo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' alisema timu yake imejiandaa kucheza soka safi kwa kuwa ndio utamaduni wa klabu yao pamoja na yeye amekuwa muumini wa 'samba'.

"Kama timu tumejiwekea malengo yetu, tumefanya usajili mzuri wa kutufikisha kwenye malengo, tumejipanga kuchukua ubingwa lakini tukicheza soka kama ilivyo utamaduni wa klabu yetu, tuko tayari kwa Ligi Kuu," alisema Robertinho.

Kocha wa Singida Fountain Gate, Hans van der Pluijm, alisema hatarajii michezo rahisi msimu huu kwa sababu timu nyingi zimefanya maboresho ya vikosi vyao kwa kusajili wachezaji wenye ubora.

"Itakuwa ligi yenye ushindani, kila timu imepata muda mwingi wa maandalizi na zimesajili wachezaji kuimarisha vikosi vyao, kwangu mimi kikubwa ni kuwafanya wachezaji wangu waendelee kucheza katika ubora wa hali ya juu katika kila mchezo," alisema Pluijm.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >